


DINI YA YEZEBELI

 Hebu na tuendeleo kusimama kwa muda kidogo tu, wakati tukimtolea Mungu shukrani kwa ajili ya jambo hili. Na tuinamishe vichwa vyetu.

Baba yetu Mtakatifu na mwenye rehema, Mungu, tunafurahi sana ya kwamba Wewe ni Mungu, na msaada wa karibu katika wakati wa shida. Tunakushukuru kwa yale uliyotufanyia. Kamwe hatuwezi kueleza, kutoka mioyoni mwetu, jinsi tunavyothamani jambo hili, na jinsi unavyokuja kutuokoa tunapokuwa katika shida. Tumejifunza, kwa miaka mingi, kukutumainia na kukuamini Wewe.

Nami ninaomba, alasiri ya leo, Bwana, ya kwamba utamwaga baraka Zako juu ya watu hawa. Jalia kusiwe na mtu aliye mnyonge miongoni mwetu wakati ibada hii itakapokwisha. Kama kungekuwako na mmoja hapa ambaye si sawa mbele za Mungu, jalia nguvu zilizomfufua Yesu kutoka kaburini, ziihuishe miili yao ipatikanayo na mauti, Bwana, na nafsi zao, na kuzielekeza Kwako. Tujalie, Bwana. Wale wasio na Roho Mtakatifu, jalia hii iwe siku moja iliyo kuu ambayo kamwe hawataisahau, na iwe siku ambayo Mungu atamwaga Roho Wake juu yao. Tujalie, Bwana. Tusamehe dhambi yetu.

Tunaomba ya kwamba utambariki Ndugu Sullivan, rafiki yetu mpendwa na wa thamani, na mawazo yake kwa ajili ya watu, na kujaribu kuwaletea kila uwezekano awezao, kuwasaidia. Naomba ya kwamba utambariki Ndugu Sullivan.

Bariki wahudumu kote nchini, kila mahali. Jidhihirishe kwao kwa wingi sana, Bwana. Jalia wasimame kishujaa mimbarani na kulitangaza Neno la Mungu, kwa kuwa tunaishi katika saa za kumalizia za historia ya ulimwengu huu. Jalia wema Wako utufunike katika nyakati hizi. Kwa kuwa tunaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

Mnaweza kuketi.

Nina shukrani sana kwa ajili yenu enyi watu, na kwa Mungu, kwa ajili ya jambo hili. Ndugu Sullivan alichukua jukumu. Unaona, haingekuwa ni sawa kwa Ndugu Sullivan kufanya jambo hilo, kwa hiyo tulikuwa tumejitayarisha kujiandaa kwa ajili ya jambo hilo. Tunakushukuru kwa ajili ya wema wako.

² Na, sasa, kwa ajili ya—ya matoleo ya upendo, ni... haikuwapasa kufanya jambo hilo. La, hilo halikuwa ni jambo la lazima. Mnaona, ninii tu... wanalipia matumizi, hoteli na chakula, tulichokula, na hilo ndilo tu lililokuwa la lazima. Lakini asanteni, sana kwa wema wenu, na hayo yataenda kusaidia umishenari na kuwaleta watu kwa Mungu. Hakutakuwa na sigara zo zote zitakazonunuliwa kwayo, wiski

yo yote, hakuna cho chote kilicho kibaya, yatatumiwa kwa mambo mema. Nami ninaomba ya kwamba Mungu ataweka matoleo hayo katika akaunti yenu huko juu, na kuyazidisha mara elfu kumi, kila dola, ama—ama peni, ama hela ambayo umetoa kwa ajili ya ibada hii.

³ Na, sasa, ninataka kushukuru jeshi la Marekani kwa kuturuhusu kutumia jengo hili kuketi humu, kufanya ibada hizi. Kwa kweli ninawashukuru kwa moyo wangu wote.

⁴ Na kama nijuavyo mimi, Ndugu Sullivan alisema kila kitu kitalipiwa sawasawa. Hatujaondoka kamwe katika jiji lo lote hata hivyo, tukiwa tunadaiwa hata senti moja, bali kila kitu kilishughulikiwa; hatuamini kamwe katika jambo lingine lo lote. Haikupasi kudaiwa na mtu ye yote, huna budi kulipa deni lako na kuwa mwaminifu. Na kama unadaiwa na mtu fulani, nenda ukawaone uso kwa uso na kuwaambia ya kwamba wanakudai, lakini wakupi muda kidogo, nawe utalipa deni hilo. Unaona? Daima, hilo ni zuri zaidi. . . .Hiyo ni tabia nzuri ya Ukristo: kuwa mwaminifu, mkweli.

⁵ Unapaswa kuishi yale tu unayozungumzia. Kama huyaishi wewe mwenyewe, ungewezaje kumtarajia mtu mwingine kuyaishi, unaona. Kwa hiyo ninyi ni nyaraka zilizoandikwa, zinazosomwa na watu wote, kwa hiyo daima iweni waaminifu, wenye haki, wakweli. Semeni kweli, haidhuru inaumiza jambo fulani jinsi gani. Semeni kweli, kwa vyo vyote vile, maana daima unaweza kusema jambo hilo vivyo hivyo kila mara. Na kama ukisema uongo, itakubidi kuzunguka maili milioni moja, na hata hivyo itakubidi kurudi kwenye uongo huo tena; na ndio tu ufanye jambo baya sana. Uwe tu mwaminifu, nawe kila wakati unaweza kulisema vile vile lilivyo kwa maana ni kweli.

⁶ Hivyo ndivyo ilivyo na Biblia. Liseme jambo tu jinsi Biblia inavyolisema, usikubaliane nalo, liseme tu namna hiyo, ninii tu. . . imeandikwa papa hapa na—na unaweza kuelekeza kidole chako kwenye jambo hilo. Ni—ni. . . hivyo ndivyo unavyomshinda Shetani. Shetani alimwambia Yesu, “Kama Wewe ni Mwana wa Mungu, hebu na tuone ukifanya muujiza. Watu wanasema Wewe ni ‘mfanya miujiza.’ Geuza mawe haya yawe mkate, na hebu tuone. Wewe una njaa.”

⁷ Yeye akasema, “Lakini imeandikwa, ‘mtu hataishi kwa mkate tu.’” Unaona? Yeye alichukua Neno la Baba na kumshinda Ibilisi, papo hapo aliposimama. Kwa hiyo unaweza kufanya jambo lile lile, kumshinda Ibilisi kwenye ardhi yake, kwa Neno la Bwana.

⁸ Basi, daima nitatoa shukrani kwa Ndugu Sullivan. Hii ni. . . Samahani kwa tamshi hili: nafikiri walipomtengenezea utaratibu Ndugu Sullivan Yeye alitupilia mbali mpango huo. Hakuna mtu kama yeye. Kuna mtu mmoja tu niliyepata kukutana naye maishani mwangu aliyenikumbusha juu ya

Ndugu Sullivan, huyo alikuwa ni E. Howard Cadle. Sijui kama yeye alipata kumjua ama la, kutoka ninino—kutoka... Ndugu Cadle alikuwa ni mvulana mzuri tu wa mashambani kama Ndugu Sullivan. Naye angetumbukiza mikono yake ndani kabisa ya mifuko yake mpaka mishipi ya kushikilia suruali yake ikavutwa chini sana, naye anazungumza amegeuza kichwa kando, na alikuwa ni E. Howard Cadle yule yule tu. Na kwa hiyo mimi ni—mimi ninashukuru sana kuwa na Ndugu Sullivan kama rafiki na ndugu katika Injili. Nami ninaomba ya kwamba Mungu atambariki yeye na maskini kanisa lake dogo juu hapa, mke wake wa thamani, wapendwa wake.

⁹ Na kwenu ninyi, wahudumu wengine mliopo hapa, kwenu ninyi pamoja na kusanyiko lenu, wahubiri wa Full Gospel, juu ya mambo madogo ya kidini ya Maandiko tunaweza tusikubaliane sisi kwa sisi. Mimi sikubaliani na mke wangu juu ya mambo fulani. Na mnajua tunatofautiana juu ya nini? Yeye anapenda sambusa ya tofaa nami napenda ya cheri, kwa hiyo hatukubaliani. Nami nitawaambia vile ninavyofanya na yangu: napenda kipande kizuri na kikali cha sambusa ya cheri (sasa hivi ningeweza kuila) na kumiminia siagi juu yake, halafu niimiminie molasi juu yake; na, ndugu, una kitu kinachostahili kuliwa! Mke wangu anaogopa. Ninafikiri anaogopa hizo kalori. Huenda akaipenda, lakini mnajua jinsi wanawake walivyo, wao wanaogopa... Wanakuwa wembamba sana hata ungeweza kuwachoma na pini na kuwakata hata ufike kwenye mfupa, na hata hivyo wao wanataka ku—wanataka kupungua. Hiyo ndiyo asili yao, nadhani, kwa hiyo kuna ninii... Na... lakini mimi ninaipenda hiyo. Sasa, hatukubaliani katika jambo hilo, mambo mengine hatuna shida. Lakini, unaona, hatukubaliani kabisa. Kwa hiyo tungeweza kuona jambo lile lile, ndugu, lakini jambo muhimu ni kwamba, tunakula sambusa, hilo ndilo jambo muhimu.

¹⁰ Kimsingi, juu ya ubatizo wa Roho Mtakatifu, na kule kuja kwa Kristo, na mambo makuu ya kiinjilisti, mafundisho ya kimsingi ya Biblia, bila shaka tunakubaliana kabisa kwa hayo. Kama kundi moja kubwa la ndugu walioungana, wasio na vizaizi vya kimadhehebu, tusio na kitu cho chote cha kutuzuia, tunatembea kuelekea Kalvari kama jeshi moja kubwa, pamoja.

¹¹ Kama ninaweza wakati wo wote kuwa msaada kwenu, nitafurahia kufanya jambo hilo. Nami nina hakika mngenitamkia jambo lilo hilo. Nanyi mnaweza kuwa msaada kwangu. Na hilo ndilo jambo moja mnaloweza kufanya, nijualo, ni kuniombea mimi, ya kwamba Mungu asiniachie nikosee. Ni—ni—ni... Sitaki kukosea moyoni mwangu, na—nataka kuwa sahihi, ninataka kufanya yaliyo mema. Kwa sababu ninatambua, kama vile Ndugu Jack Moore alivyoniambia wakati mmoja, alisema, “Ndugu Branham, nisingesimama mahali pako hata nikipewa ujuzi wako wote, kwenye ile Siku ya Hukumu, kwa

maana Mungu atakuwajibisha mengi,” kasema, “kwa maana amekupa mamilioni ya watu mkononi mwako.”

¹² Sasa, kama ninajua itanibidi kusimama pale na kuwajibika kwa ajili ya watu hao, basi ni Injili ya namna gani ninayopaswa kuhubiri? Ni uaminifu wa aina gani, wakati ninaposhika kilichonunuliwa na Damu Yake mikononi mwangu? Na kama vile alivyonipa karama kuninii...bila shaka yo yote, mtu ye yote mwenye akili timamu angejua inatoka kwa Mungu. Na nikiwa na hiyo, kama ningemwongoza mtu fulani vibaya katika njia mbaya ati kwa sababu tu kundi fulani lilisema jambo hilo, Mungu ataniadhibu kwa jambo hilo kwenye Siku ya Hukumu.

¹³ Lakini nilipoona lile ono, hapa si muda mrefu uliopita, na kuwasikia watu hao wakipiga makelele...Je! mlipata kile kitabu chenu kidogo jana usiku? *Sauti* ya Wa—Wafanyi Biashara. Vyema. Na katika lile ono (siku moja tutalichapisha kikamilifu, hayo si yote)...lakini katika jambo hilo, na kuona jambo hilo, nami nilisimama pale kama tu—kama tu vile ninavyosimama sasa hivi. Nami nilikuwa nikijiangalia nimelala pale kitandani, nikimwangalia mke wangu, na sasa hivi nimesimama hapa nikijiangalia mwenyewe. Na hawa hapa wale watu wamesimama hapa namna hiyo wakati niliposema, “Je! itambidi Paulo kuhukumiwa kwa Injili aliyohubiri?”

¹⁴ Kasema, “Naam.”

¹⁵ Nikasema, “Nimehubiri kila Neno jinsi tu yeye alivyohubiri.”

¹⁶ Na mamilioni wakasema kwa sauti kuu, “TUNATUMAINIA JAMBO HILO!”

¹⁷ Hivyo ndivyo ninavyotaka iwe nitakapovuka kwenda kule, unaona. Ninataka iwe namna hiyo, namna hiyo tu, kama vile tu Paulo alivyosema. Sitaki kuongeza jambo moja kwa Hayo, kuondoa jambo moja kutoka kwa Hayo. Vile Biblia ilivyosema tu, hivyo tu ndivyo ninavyotaka kuendelea nalo mbele, unaona. Na bila shaka, ninyi watu mliweke hivyo, madhehebu kila upande yataweka kizuizi dhidi Yake.

¹⁸ Na halafu, mara nyingi, ndugu wanafikiri ya kwamba mimi sina uhusiano na ndugu zangu. Mungu anajua vinginevyo, mradi tu Yeye anajua ukweli wake. Unaona? Sina uadui na hao ndugu, ni madhehebu ndiyo yanayotufanya tusiwe ndugu. Si Neno la Mungu linalotufanya tusiwe ndugu, ni madhehebu tunayojiunga nayo ambayo yanatufanya tusiwe ndugu. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo, tunapaswa kusimama wapi? Kusimama kwenye Neno, na Mungu atawavuta watu wote Kwake (hiyo ni kweli) kwenye—kwenye hilo. Kamwe msiunde madhehebu, kulifanya madhehebu, liwekeni licha ya yote hayo katika Mungu, na mwendelee tu kusonga mbele; mkiangalia mwisho tu, shikilieni imara, Mungu ataleta yaliyosalia.

¹⁹ Kuna mambo mengi sana mliyonifanyia, nami ninayathamini. Sasa kama ninaweza kuwasaidia, kwa kuwapa kitambaa cha maombi ama cho chote kile. Sasa, msiniulize juu ya fundisho, kwa maana si—sitamani kufanya hivyo. Watu wengi sana huniandikia maswali kuhusu ndoa na talaka na kadhalika, mambo ambayo ni matatizo kanisani. Mimi daima huwarejeza nyuma, na kusema, “Muulize mchungaji wako.”

²⁰ Watu wameniandikia barua hapa na kusema, “Na jambo *hili* je?” Na jambo *lile* je? Ninairudisha barua hiyo, utaipata. Mwone mchungaji wako katika mambo madogo kwa sababu, hata hivyo, yeye ndiye mchungaji wako. Unaona, yeye ni ninii—yeye ndiye ambaye Mungu amemtuma kukuchunga. Nasi huenda tusikubaliane juu ya jambo hilo, ndipo jambo hilo linaleta mafarakano kanisani kwenu. Hatutaki jambo hilo. La! La! Tunawatakeni tu muache kufanya mambo ambayo ni dhambi, mambo yaliyo nje ya Biblia, na mwendelee kusonga mbele kwa Mungu. Mnaona? Na kama ukisababisha ubishi mdogo na vitu kama hivyo, hilo linalisumbua kanisa. Kwa hiyo, afadhali mchungaji wako akwambie juu ya ndoa na talaka, na mambo *haya* na mambo *yale*, hebu na afanye jambo hilo. Yeye ni mtumishi wa Bwana pia, naye ametayarishwa kufanya jambo hilo.

²¹ Mnamkumbuka yule Msamaria mwema aliyekuta yule mtu aliyejeruhiwa? Yeye alimleta mpaka nyumba ya wageni (hiyo ni kanisa) na kumpa huyo mtu pale peni mbili, akamwambia kama alihitaji zaidi yeye angemlipa atakapokuja. Kwa hiyo, yeye ana peni mbili, yeye anaweza kukutibu kama yeye ni mtu wa Mungu. Kama yeye ni mtu wa Mungu anayesimama kwenye Neno la Mungu, yeye—yeye ana kile alichopewa na Mungu: Roho na Neno. Hiyo ni kweli? Tunapaswa kuabudu namna gani? Katika Roho na Kweli. Nalo Neno ni Kweli. Hiyo ni kweli?

²² Sasa, asanteni kwa wema wenu, tena. Na sasa, nimechoka sana, na nimechoka sana alasiri ya leo, sikusudii kukaa tena kwenye hoteli mradi nikali hai. Shamrashamra za walevi, na usiku kucha, wakipigapiga milango na kupiga makele, na wanawake... Loo! niliketi macho tu, usiku kucha, nikiangalia nyota. Na kwa hiyo si—sitaki kukaa kwenye hoteli tena. Nitaenda kwenye moteli. Nitajipatia lori kusudi nipate kulala ndani yake, huko nje sakafuni mahali fulani. Nitalipata, nijinunulie hema na mfuko wa kulalia, ama mahali fulani ambapo ninaweza kuwa peke yangu, mahali fulani. Hiyo ni kweli.

²³ Ni lenye dhambi sana, taifa hili, si ajabu! Limetobokatoboka, na limeoza kabisa. Papa hapa jirani na hapa, kwenye mkoa wenu... Si mkoa huu peke yake, kila mahali. Papa hapa, miaka michache iliyopita, nilikuwa katika m—katika mkutano wa dini hapa mkoani, jiji kubwa. Na usiku huo kundi la kidini, kanisa la kiothodoksi lenye vijana, walikuwa

na mkutano. Si—sijapata... Nimekuwa huko Afrika nikaona uchawi halisi na kila kitu, sijawahi kusikia kamwe kitu kama hicho. Na asubuhi yake, (siwezi kuwaambia jambo lenyewe hasa, tuko katika mkutano uliochanganyika)... vimetapakaa sakafuni, vitu vya mambo machafu yaliyokuwa yamefanywa, chupa za wiski kila mahali. Na hao watoto wadogo, wavulana na wasichana katika chumba kimoja usiku kucha, wako pamoja. Na kesho yake asubuhi, “baba mtakatifu” ameketi hapo, nao wanamjia wakimsujudia namna hiyo; chini ya Jina la Yesu Kristo!

²⁴ Je! nimeingia kichaa? Hivi—hivi nimeshikwa na nini? Siwezi kabisa kuvumilia mambo hayo! Ni... kitu fulani kinanitetemeshia vibaya sana ninapooona jambo hilo. Je! hilo ni jambo la kumwakilisha Bwana wangu Yesu? Shamrashamra ya walevi, na vitu vya uasherati ambavyo... vimetumiwa na hao vijana wa kiume na wa kike, viko kwenye sakafu na katika vikapu vya takataka, na chupa na... Loo, jamani, majonzi! Ungeweza kuita jambo hilo ni Ukristo? Si ajabu ulimwengu uko katika angahewa la dhambi. Vema, mwenye dhambi anasema nini anapoangalia jambo hilo? Maelfu yao.

²⁵ Hao wasichana wadogo wamelewa sana hata hawakuweza hata kidogo kusimama, na wamekuwa huko kwenye chumba usiku kucha pamoja na hao wavulana, na mazungumzo yaliyo machafu sana uliyopata kusikia maishani mwako. Niliweka mito juu ya kichwa changu namna *hii*, nikijaribu kulala usingizi. Huko nje sakafuni, wamelewa, na wanakimbia huko na huku sakafuni namna hiyo, ati wa kidini!

²⁶ Sasa, ninaweza kutarajia hawa watu wenye dhambi kama hao, sasa, wanaojiita waungwana, hapa nje kwenye mchezo wa kufingirisha tufe. Mmoja wa watoto wangu angalianza kuelekea kwenye uwaja wa mchezo wa kufingirisha tufe, ningemfukuza nchini. A—ha. Ati mnaita huo ni uungwana, huo si uungwana. Kile jambo hili... Kama unataka kuwa muungwana, jiweke sawa na Mungu. Kweli.

²⁷ Ninataka kuwasomea, Neno moja tu kutoka katika Biblia. Unaona, maneno machache ninayotaka kusoma hapa kwa ajili ya somo, yanayopatikana katika mlango wa 17 wa Wafalme wa Kwanza, kifungu cha 1:

... Kama Bwana, Mungu wa Israeli, aishivyo, ambaye ninasimama mbele zake, hakutakuwa na umande wala mvua miaka hii... kwa neno langu. Wafalme wa Kwanza, mlango 1... mlango wa 17, kifungu cha 1.

²⁸ Kama ninaweza kukutumia kitambaa cha maombi, wakati wo wote, niandikie tu; katibu wangu hapa, ambaye yupo sasa, Ndugu Maguire. Ni wangapi wamewahi kupata kitambaa cha maombi kutoka kwetu? Hebu tuone mkono wako. Simama Ndugu Jim. Ninataka kuona kwa... wewe, na mke wako pia.

Huyu hapa katibu wangu na mke wake, wale wanaofanya kazi, ambao wametuma... Hao ndio yule mvulana na yule msichana wanaokutumia kitambaa chako cha maombi toka kwenye mkutano, wote wawili ni Wakristo waliowekwa wakfu. Na ile sauti, ile sauti ndogo na tamu mnayoisikia kwenye simu mnaponipigia mimi simu, hiyo ni ya maskini bibi yule anayeketi pale, mke wa mwanamume yule. Baba na mama yake, na hao wengine, wako hapa pamoja nasi leo; na—na wapendwa wao, wote wako hapa. Kwa hiyo... Na kisha mnajua katibu wangu wa kazi, Ndugu Mercier, Ndugu Leo Mercier, yeye yuko hapa mahali fulani, na Ndugu Gene Goad. Na kwa hiyo kama tunaweza kuwatumieni kitambaa cha maombi, wakati wo wote, lo lote tunaloweza kufanya, kuwaombeeni kwenye simu; lo lote tunaloweza kufanya, tutalifanya.

²⁹ Mtu huyu anayeonekana mgeni aliyeshika fimbo mkononi mwake, hatua zake imara, macho yake yakimetameta kwa Utukufu wa Mungu, ndevu zake zikipepea shavuni mwake, kipande kichakavu cha ngozi ya kondoo alichovaa, alikuwa akipiga hatu zake kishupavu tu alipokuwa akienda zake huko Samaria. Hakuwa mtu wa kuvutia macho sana, bali alikuwa na BWANA ASEMA HIVI kwa ajili ya taifa hilo kuu la Israeli. Naam, Eliya Mtishbi, nabii wa Bwana. Hakuwa wa kuvutia macho, bali alikuwa na Neno la Bwana.

³⁰ Hakuogopa kusimama mbele za mfalme, kwa kuwa amekuwa Uweponi mwa aliye mkuu kuliko mfalme, alikwisha kuwa Mbele za Yehova. Kwa hiyo, yeye alijua mahali alipokuwa amesimama. Na hapo alipoenda mbele za mfalme yeye hakubabaika maneno wala kusitasita, yeye alijua alichokuwa akizungumzia. Angeweza kumwambia mfalme, “BWANA MUNGU WA ISRAELI ASEMA HIVI, ‘Hakutakuwa na mvua wala umande ila kwa neno langu.’” Kwa nini alisema hivyo: “Ila kwa neno *langu*. Ila kwa neno *langu*”? Kwa sababu alikuwa na Neno la Bwana, alikuwa nabii, na nabii ana Neno la Bwana.

³¹ Ni jambo la kushangaza kuona usambamba kati ya Israeli ya Agano la Kale na Marekani sasa. Yote mawili yalikuwa ni mataifa makuu. Yote mawili yalikuwa yameanzishwa, na watu wake walikuwa wameenda kule, kwa sababu ya mateso ya dini.

³² Israeli ilikuwa imeteswa na Farao na ilikuwa utumwani kwa mamia ya miaka, ambapo walikatazwa kumwabudu Mungu wa kweli na aliye hai, nao walikuwa wamenyimwa uhuru huo; nao wakawa watumwa. Lakini Mungu alikuwa amewapa ahadi katika Biblia Yake, ama katika Neno Lake, na kwa manabii Wake, ya kwamba angewapa nchi. Nao wakaingia katika nchi hii na kuwafukuza wenyeji wa nchi hiyo, nao walikuwa wamemiliki urithi wao, kwa maana Mungu alikuwa na kusudi la kufanya jambo hilo.

³³ Na vivyo hivyo ndivyo imekuwa taifa hili letu kuu. Tulikuja hapa, na kwenye Plymouth Rock taifa hili lilianzishwa juu

ya uhuru wa kuabudu kwa sababu wahenga wetu walikuwa wameyakimbia mateso ya Kirumi chini ya mfumo wa Yezebeli wa kisasa, nao walikuwa wamekuja huku na kustahimili mateso makuu na ufiamani chini ya mfumo huo wa uongo wa Yezebeli. Na kulingana na Biblia, kwenye Ufunuo, mlango wa 13, Mungu aliwaahidi raha mstarehe, na mahali, kwa kuwa yule mwanamke alichukuliwa hata jangwani ambako alilishwa kwa wakati, wakati, na nusu wakati. Mungu alikuwa ameipa Marekani ahadi, ama kanisa (kwa yule mwanamke), kuja kwenye nchi hii.

34 Je! uliona Ufunuo 13? Wanyama hao wengine wote walikuwa wametoka katika bahari, maji; Ufunuo 17:17, ilisema, “Maji uliyoyaona ni jamaa na umati wa watu.” Wanyama hao wengine wote, walitoka majini, jamaa na umati wa watu. Lakini wakati Marekani ilipotokea, “Ilitokea kutoka katika nchi ambako hakukuwako na watu.” Basi kumbukeni, wakati ilipotokea, ilionekana kama mwana-kondoo mchanga.

35 Sasa, mwana-kondoo ana pembe mbili, na hizo ni nguvu za kisiasa na nguvu za kidini. Lakini wakati zilipoungana, kumbukeni, ndipo mwana-kondoo huyo alinena kama yule joka alivyofanya mbele yake; na huyo joka alikuwa ni Rumi.

36 Wakati yule joka aliposimama mbele za yule mwanamke apate kumla mtoto wake mara alipozaliwa, lile joka jekundu. . . Ni nani aliyesimama mbele za mwanamke Israeli, kumla yule mtoto mara alipozaliwa, na akasababisha mateso na kuwaua watoto wote tangu umri wa miaka miwili kwenda chini? “Rumi, yule joka, alisimama mbele za yule mwanamke kumla mtoto wake mara tu alipozaliwa.”

37 Halafu, tunaona, ya kwamba nchi hii ilianza kama nchi huru, na ilikuwa. . . ilikuwa na mwana-kondoo, ambalo linamaanisha Mwana-Kondoo wa Mungu. Lakini, baada ya kitambo kidogo, mfumo uu huu tulio nao, ulinena kama yule joka na kutumia uweza wote wa yule joka mbele yake.

38 Yanalingana, moja kwa lingine, kabisa. Na kumbuka wakati hizi. . . Israeli ilitokea na kuchukua nchi ya uenyeyi wao Palestina, ikawafukuza wenyeji wote wa nchi hiyo na kuimiliki nchi hiyo. Sisi tuliingia na kuitwaa kutoka kwa Wahindi, tukawafukuza na kuimiliki nchi. Mungu alikuwa na kusudi kwa jambo hilo. Mungu alikuwa akitaka kuonesha ulimwengu yale angeweza kufanya na kundi do—dogo la watu waliotaka uhuru, na uhuru wa imani, wa kumtumikia Mungu.

39 Walimtendea nini Israeli? Alimfanya Israeli kuwa taifa lililo na nguvu kuliko yote ulimwenguni, nalo likakaa namna hiyo mpaka lilipotoka katika mapenzi ya Mungu. Yeye alifanya nini na Marekani? Alilifanya taifa lililo na nguvu kuliko yote ulimwenguni mpaka linatoka kwenye mapenzi ya Mungu. Yanaenda sambamba, moja kwa lingine, hasa.

⁴⁰ Wakati Israeli walipokuja katika nchi ile, walikuwa ninii—walikuwa ni watu wakuu kwa sababu walikuwa na uongozi maarufu. Waliongozwa na watu waliomcha Mungu, kama vile Daudi, Mfalme Sulemani. Ulimwengu mzima uliwaogopa, nao wakafurahia majaliwa hayo ya kutokuwa na vita, matatizo, nao wakiishi chini ya nguvu za Mungu, mpaka watu kutoka kote kote katika ulimwengu uliojulikana wakaja kuwaona. Mungu aliwapa karama ya utambuzi, kipawa hicho kilikuwa juu ya Sulemani. Ndipo malkia wa Kusini, kutoka . . . malkia wa Sheba akaja kutoka mbali ng'ambo ya pili ya Jangwa la Sahara (ilimchukua miezi mitatu) kusikia tu hekima ya Sulemani. Na wakati alipoona ya kwamba Sulemani aliweza kutambua roho, na kumjulisha siri za moyo wake, akasema, “Yote niliyosikia kukuhusu wewe yalikuwa ni kweli, na zaidi sana.” Yeye alikuwa ameshawishika ya kwamba huyo alikuwa ni Mungu.

⁴¹ Na Marekani, juu ya msingi wa wahenga wetu waliokuja hapa kwa ajili ya uhuru wa imani. . . Tulikuwa na watu wacha Mungu siku hizo, kama viongozi: George Washington, Abraham Lincoln, watu wenye sifa nzuri, watu wa Mungu. Marekani ilikuwa Marekani, siku hizo.

⁴² George Washington, hapa katika Valley Forge, kabla ya kuvuka Delaware, akiomba usiku kucha, mpaka akalowa maji hata kiunoni, akipiga magoti katika theluji. Na kesho yake asubuhi wakati Wamarekani walipoanza kuvuka, kulikuwako tu na kama asilimia ishirini yao waliokuwa na viatu vya kuvaa, Jeshi la Marekani. Lakini walikuwa na msimamo, walikuwa na jambo fulani lililowapasa kupigania. Hawakujali kilichokuja ama kilichoenda. (Wakulima waliingia, akasimamisha plau lake na kumwondoa maksai wake, akachukua bunduki yake akaenda kupigania alichojua kilikuwa ni uhuru wake.) Na kesho yake, naamini ilikuwa kesho yake, matundu manne ama matano ya risasi (risasi za gobori) zilipitia kwenye koti lake na kofia yake wala hazikumgusa.

⁴³ Watu wa Mungu, ambao walianzisha taifa hili, watu mashuhuri! Si ajabu waliandika:

Nchi yetu daima na ing'ae
Kwa nuru takatifu ya uhuru;
Tulinde kwa nguvu Zako,
Mungu mkuu, Mfalme wetu!

⁴⁴ Muda fulani uliopita, nilizungumza na mzee mmoja kule Corydon, Indiana. Aliniambia juu ya wakati ambapo ikulu ilikuwa huko Corydon, na jinsi alivyo-. . . akaeleza jinsi alivyosafiri kwenda huko kwa gari la ng'ombe akamsikie ga—gavana akizungumza. Basi yeye pamoja na gavana ndio watu wawili pekee waliokuwa wamevaa suti ya vipande viwili. Kasema ya kwamba yeye alifuga kondoo na kuwakata manyoya, na kusafisha sufu yao, dada zake wakaifuma wakamtengenezea

koti ya kuvaa na suruali yake. Na maskini mzee huyo akiketi hapo, wakati huo akiwa na kama umri wa miaka themanini na mitano ama tisini, kavuta ndevu zake namna *hiyo*, na kusema, “Billy, huo ndio wakati ambapo ‘Marekanii’ ilikuwa ni ‘Marikanii.’”

⁴⁵ Nikamwangalia maskini jamaa huyo, nami nikawaza, “Jamani, wewe. . . baadhi ya vijana hawa wasingeamini jambo hilo, bali unasema kweli.”

⁴⁶ Ilikuwa kwa Israeli baada ya msingi huu wote wa kiungu? Walianza kutokujali. Walianza kufikia mahali ambapo wao, vema, hawakujali kile kilichokuwa kinaendelea. Walianza kuwa wazembe katika kumwabudu Mungu, ingawa walishikilia namna fulani ya dini kama tu tuliyo nayo. Walikuwa na mfano wa utauwa. Lakini wakaanza kujiachilia na watu wao, na—na wakaanza kuingiza maasi mbalimbali kanisani mwao. Ibada za Baali zikaanza kuingia kisiri, na Israeli wakashikwa na wazimu wa anasa, ulevi, na mambo kama hayo, na hatimaye wakamwingiza kiongozi asiyemjua Mungu; Ahabu, aliyemfuata baba yake. Na baba yake alikuwa ni mtu asiyemcha Mungu, tajiri, bali ni mtu asiyemcha Mungu. Naye akafanya kila dhambi, zaidi kuliko mtu ye yote aliyemtangulia alivyopata kufanya. Bila shaka Israeli, katika ulevi wao wa kupindukia, walimweka mtu wa namna *hiyo*, na kumweka kwenye kiti cha enzi kuwa mtawala juu yao. Walidhani ilikuwa ni sawa. Kama tu vile Wamarekani wengi wanavyofanya siku hizi, “Yeye ni mwanasiasa mzuri, kwa *hiyo* inaleta tofauti gani? Haitaleta tofauti yo yote, kwa maana yeye ni mwanasiasa mzuri.”

⁴⁷ Wamarekani wengi, wengi kupita kiasi, wameuza haki yao ya mzaliwa wa kwanza, kama Mmarekani, na kusema, “Inaleta tofauti gani, mradi tu mtu unapata dola chache za ziada kutoka serikalini na kuishi?” Walijiua kwa posho, na kwa tamaa mbaya na uchu wa ulimwengu wenye dhambi, na wamesahau jambo lile lile lililotufanya tushukie Plymouth Rock. Wamesahau urithi wetu, nao wakaenda na wakajiua kwa umati wa watu walioshikwa na wazimu wa anasa. Kama ilivyokuwa katika siku za Israeli, ndivyo ilivyokuwa, Marekani imechukua barabara ile ile, moja kwa moja kwenye njia ile ile, anasa!

⁴⁸ Baada ya kitambo kidogo, serikali ikaidhinisha dhambi: “Mradi tu mlikuwa na sinagoga, imeleta tofauti gani?” Hivyo ndivyo Marekani ilivyofanya hasa. Nasi tukaanza kujiandaa pamoja na kuunda vikundi vidogo, na kutenda dhambi zaidi, tukazama dhambini zaidi, tukazama dhambini zaidi. Laiti tungalidumu na misimamo ile ile iliyotuleta huku! Dhambi ilianza kunyemelea katika makanisa kama tu ilivyofanya wakati ule. Wanawake wakaanza kukata nywele zao, wakivaa nguo chafu, wakizifupisha kila mwaka. Nao wanaume wakaanza kufanya *hivi*, *vile*, na *vinginevyo*, na kucheza karata na kufanya michezo ya bahati nasibu kanisani, na kuwa wa kilimwengu

tu kama walivyokuwa, wameingia kichaa cha anasa, walevi wa kupindukia.

⁴⁹ Wahudumu wakihitimu kutoka seminari, na askofu akisema, “Hubirini, enyi vijana, cho chote mnachotaka. Nionavyo mimi, damu ya Yesu Kristo ilikauka miaka elfu moja mia tisa iliyopita.” Mpaka kanisa likawa si kitu ila madhehebu, kama loji. Naomba kamwe usisahau alasiri ya leo! Likawa kama loji, ulimwengu ukaanza kunyemelea na kuingia ndani, wahudumu wakaanza kudhoofika kama tu vile walivyofanya katika siku za Ahabu. Wenye dhambi, wameoza kabisa, ndipo hilo likaendelea na kuendelea upesi lilivyoweza kwenda.

⁵⁰ Ingawa Mungu aliwatumia nabii baada ya nabii, na kwa rehema za upendo Yeye aliwasihi watu, nao wakalipa hilo kisogo. Walitaka kufanya watakavyo, walikuwa ni Waisraeli, huru, walikuwa ni taifa kuu, wahenga wao walifanya *hivi* na vile. (Daudi na Sulemani), waliweza kufanya walivyotaka kufanya. Jambo lile lile ambalo tumejiwekea msingi nalo, kweli kabisa; yale Washington, wahenga wetu, na kile walichotetea. Lakini, ndugu, tuko maili milioni moja mbali kutoka kwenye mambo hayo; makanisa yetu yako hivyo, maili milioni moja.

⁵¹ Maskini... Kanisa la Kimethodisti leo, ukilinganisha na vile Methodisti lilivyokuwa! Vile Pentekoste ilivyo leo, na vile ilivyokuwa! Vile Baptisti ilivyo leo, na vile ilivyokuwa! Laiti tungalikuwa na wakati wa kurudi nyuma, na kunena juu ya John Smith na wengi wa wale watengenezaji wa mwanzoni. John Smith alisema, kabla hajafa, alisema, “Jambo la kuchukiza sana ni kwamba wanawake wa Kimethodisti wameanza kuvaa pete za dhahabu vidoleni mwao.” Wamethodisti! Angesea nini leo hii akiwaona wamekata nywele zao, na rangi uso mzima, wakivaa kaptura? Ni kwa sababu ya dhambi!

⁵² Mungu amefanya nini Marekani? Ametuma ufufuo baada ya ufufuo, ufufuo baada ya ufufuo. Wahudumu wamehubiri Neno, wakajaribu kuwaita watu wamrudie Mungu. Na watu walifanya nini? Jambo lile lile Israeli walilofanya, wamekataa Neno! Wakawadhihaki! Wakawaita “watakatifu wanaojifingirisha”! Wakawatupa gerezani!

⁵³ Kama mmoja wa dada zangu na mmoja wa ndugu zangu, kutoka katika kanisa hili leo, wangelisimama kwenye ile hoteli jana usiku na kuinua mikono yao na kumsifu Mungu na kupaza sauti katika chumba hicho, wangekuwa gerezani leo juu ya jambo hilo. Bali kundi la walevi, la wajinga wenye dhambi wanaojifingirisha waliolewa chakari wanaweza kusimama pale na kupiga makelele usiku kucha; nao wamelewa, na kulaani na kunyakua nguo za wanawake wao na kufanya yasiyofaa, na kuanguka sakafuni na kupaza sauti usiku kucha, na hata wao hawawezi kusema neno hata kuhusu jambo hilo. Si ajabu tumehukumiwa chini ya mkono wa Mungu!

⁵⁴ Angalia, kuendelea na kuendelea, Mungu alituma wahudumu, wakafanya ishara na maajabu, wakithibitisha Neno Lake. Na karibu mambo yote, makasisi wengi wa kisasa walilipuuza na kufanyia mzaha kila ufufuo. Kama vile lile linalojiita Kanisa la Kristo na hayo mengine, “Siku za miujiza zimepita.” Wakijaribu wawezavyo kuyafungia mbali na hayo masalio madogo ya Mungu. Kama ilivyokuwa katika Israeli, ndivyo ilivyo leo. Mara nyingi, inambidi Mungu kuchukua watu Wake kutoka kwenye hayo mashirika na madhehebu, kuwapeleka huko nje nyikani peke yao, apate kuzungumza nao. Naye atakuwa na masalio, usijali kuhusu jambo hilo. Alifanya jambo hilo wakati huo, Yeye atalifanya sasa. Wakazidi kuendelea na kuendelea katika dhambi, wakigaagaa katika uchafu. Kwa nini? Uongozi wao, hakuna cha kuwazuia.

⁵⁵ Vema, kwa kweli, najua mataifa mengi kwamba kama wangewashika watu mitaani wamevaa jinsi tunavyovaa hapa Marekani, wangewafunga gerezani. Nilipoenda huko St. Angelo, Roma (sasa, wazia jambo hilo, duni kama huo ulivyo duni), walikuwa na kibao kule, karibu na makaburi ya St. Angelo, “Kwa wanawake wa Marekani: ‘Mnaombwa kuvaa nguo zenu na kuwaheshimu wafu.’”

⁵⁶ Kama kuna jambo lo lote linalokuchefua, ni kuona kundi la hao wanaojiita Wamarekani likiingia. Nilikuwa nimeketi chini, huko Lausanne, tulikuwa tukila steki, siku moja, mimi pamoja na Ndugu Arganbright. Kesho yake, tukarudi kwa maana kilikuwa ni chakula kizuri. Ningeweza kupata maji kule, wasingehudumia cho chote ila divai. Nami ningechukua maji, ilinibidi nibebe chupa ya maji mikononi mwangu, kila wakati, kwa maana wasingekuhudumia maji mezani. Ndipo nikaenda kule, na kila kitu kilikuwa ni kizuri mpaka “Bi Marekani” alipoingia akiwa na maskini kijimbwa kichafu chenye pua la kukoroma; akiwa amevaa vito vya kutosha kutoka kwenye duka-la-hela-kumi namna hiyo, na sigara huko mwisho namna hii, akaketi pale akijifanya kitu fulani asicho; kisha akakiweka kile kijimbwa mezani, kichafu, kitu kichafu.

⁵⁷ Ni...mbwa ndicho kitu kibaya sana ambacho Mungu ananena habari zake. Hata zaka kutokana na hao haziwezi kutolewa katika nyumba ya Mungu. “Ni kama kahaba, zaka ya kahaba,” Biblia ilisema. Na, hata hivyo, haya basi. Wao watatumia uzazi wa majira na kulipa dola elfu moja, karibu elfu moja, kwa maskini kijimbwa kidogo; na kukiongoza huku na huko kukipa upendo wa mtoto, kusudi apate kuzurura usiku kucha, naye atatumia uzazi wa majira.

⁵⁸ Ni nini kinachongojea ila mchafuko! Huenda msisikie sauti yangu tena, lakini ninawatakeni kukumbuka jambo hili: tuko katika wakati wa mwisho!

⁵⁹ Hapo, tunaona jambo lililotukia, kile kilichotendeka. Hatimaye, ile saa iliyo *kuu* ikaja: Ahabu akachaguliwa, na

alipochaguliwa, akamwoa Yezebeli; yule mwanamke mchafu sana aliyeiongoza Israeli yote katika uzinzi. Na kama vile Israeli ilivyofanya wakati huo, mbona, hii... Hapana budi walikuwa katika hali ya kuanguka, kuachilia jambo kama hilo litukie katika taifa lao. Sheria zinafanywa na watu kwa ajili ya watu, nasi tumefanya jambo lile lile!

⁶⁰ Kulikuwa na wakati ambapo Marekani isingeninii... walimkataa yule kahaba mchafu, yule malaya wa kale aliyelewa kwa damu ya wafiaimani (akawaua)... Na sababu ya kutoroka kwao hapa: kwa ajili ya uhuru, wasingeweza kuvumilia kitu kama hicho. Inaonesha tuko katika hali ya kuanguka, taifa zima, kuchagua kitu kama hicho. Loo, bila shaka, sasa ninyi... baadhi yenu ninyi Wademokrati waaminifu sana mtafikiri hivi, ya kwamba "Loo, vema, yeye ataninii—yeye atakuwa kiongozi mzuri wa siasa." Hilo linaweza lisikike sawa kwenye hoja, kwa mtu wa mwilini. Lakini kwa Neno la Mungu na kwa mtu wa kiroho, halina maana. Bila shaka halina, dola chache za ziada na kodi kidogo ama kitu kama hiki kupunguza.

⁶¹ Na tuna wakati mgumu, wamishenari wetu huko kwenye huduma leo, kwa sababu sasa tunahesabiwa kuwa ni taifa la Kikatoliki. Kwa nini, hakika, Urusi inahesabiwa kwamba ni ya kikomunisti kwa sababu wao wana kiongozi wa kikomunisti. Uchina Nyekundu inahesabiwa kuwa ni komunisti kwa sababu wana kiongozi wa kikomunisti. Sisi tunahesabiwa kuwa taifa la Kikatoliki kwa sababu eti tuna kiongozi Mkatoliki.

⁶² Loo, wakati Ahabu alipokuwa kwenye kiti cha enzi... Unasema, "Yeye ndiye aliye kwenye kiti cha enzi." Hiyo ni kweli, lakini Yezebeli ndiye aliyekuwa kiongozi nyuma ya kiti hicho cha enzi. Yeye ndiye aliyekuwa anaongoza. Angalia jinsi alivyochukua sheria za nchi na kuzigeuza, na kwa manufaa yake mwenyewe na kwa tamaa, na akafanya Ahabu afanye jambo hilo kwa sababu alikuwa ameolewa naye. Na hivyo ndivyo ilivyo kwa kiongozi wetu siku hizi. Sisemi yeye si mtu mzuri, lakini angalia ni kitu gani kilicho nyuma yake: yule kahaba, kitu kile kile kilichotufanya tukimbilie hapa (kuwa Marekani); Kanuni zile zile ambazo Marekani imejengwa juu yake. Sisi, kwa kuchagua kwa hiari yetu, tulichagua kitu kama hicho.

⁶³ Sasa mnaona ni kwa sababu gani sauti yangu itakomeshwa hivi karibuni sana. Lakini mtu fulani atajua! Naam! Kwa nini? Ufunuo 2:20, alijiita "nabii mke." Wewe ngojea tu wimbi la dhambi likitokea sasa. Wewe ngojea kiini kikienda moja kwa moja kwenye kiini. Wewe angalia vitu vya kisasa, angalia vitu viovu vikitokea makanisani. "Na, hatimaye, kutatokea mateso," Biblia inasema hivyo, BWANA ASEMA HIVI! Bila shaka, kutakuwa na mateso.

⁶⁴ Basi ni jambo gani litakalotukia? Kama tu vile ilivyotukia wakati huo, ndivyo itakavyokuwa sasa. Yeye alikuwa ndiye

nguvu iliyoko nyuma yake, yeye ndiye aliyeiongoza. Soma ninii . . . Ninaamini ni ninii ya kumi na sa- . . . mlango wa 17 ama 18 hivi, mahali fulani hapo, utaona yale Yezebeli aliyofanya: jinsi alivyomchukua Ahabu, wala hakuweza kusema jambo lo lote juu yake kwa sababu ilikuwa ni mkewe. Angalia msingi lilimojengwa taifa hilo wakati huo, Mwisraeli aliyeanguka akiwa na mke kafiri (nyuma yake) aliyekuwa ni mwabudu wa Baali. Naye alifanya nini? Hatimaye alifanya kila kitu kuwa cha kisasa sana, na kizuri sana, nao watu walikuwa wanaishi maisha ya starehe, mpaka kanisa lote likayaendea hayo, wahubiri na wengine wote. Hivi Eliya hakusema, “Bwana, mimi peke yangu ndiye niliyesalia”? Na kama ilivyokuwa wakati huo, inalingana na siku hizi.

⁶⁵ Wote waliogopa kusema jambo lo lote. Je! si ni jambo kama lile lile siku hizi? Waliogopa kusema jambo fulani. Kwa hiyo tunaona, wao walikuwa tu wamelegea, ovyo ovyo, walevi, wakifanya maovu, wenye kichaa cha anasa, na cho chote kile, kama tu ilivyo siku hizi. Yezebeli akigeuza Maandiko hayo, . . . Yeye ali- . . . ama hizo sheria, kama—kama Yezebeli atakavyogeuzi. Kumbukeni, Yezebeli, yeye anajiita “nabii mke,” apate kuwatiisha watu, naye anasema ya kwamba yeye ndiye “sauti pekee ya Mungu duniani.” Yeye atawafanya watu wa kimwili kuamini jambo hilo bila shaka kabisa.

⁶⁶ “Kutakuja kuabudu mwanamke, katika Marekani, na huyo utakuwa ni Mariamu.” Niliona jambo hilo, thelathini . . . 1931. Mambo saba yalitukia. Ninayo papa hapa kwenye karatasi, pamoja nami, niliyoandika 1931. Jinsi ambavyo nilisema “Rais huyu, Franklin D. Roosevelt, atasababisha ulimwengu mzima, atachangia, ataelekeza ulimwengu vitani.” Haukuwa umeingia vitani bado, katika ule wakati wa kuzorota kwa uchumi. Nikasema, “Jambo lingine, . . .” Na mama yangu, Mdemokrati shupavu, kama hakuniangalia kwa ukali wakati niliposema jambo hilo. Nikasema, “Sijali kama alikuwa Mripablikan ama kama alikuwa Msoshialisti ama cho chote kile, hii ni BWANA ASEMA HIVI.” Ndipo nikasema, “Kwa kufanya jambo hili, wao wanawaruhusu wanawake kupiga kura. Na wakati watakapofanya hivyo, watafanya moja ya aibu kubwa sana taifa hili lililowahi kufanya.” Nami nikasema, “Siku moja watajutia jambo hilo.” Nao walijuta katika uchaguzi huu uliopita. Hao ndio waliomchagua yeye, wanawake.

⁶⁷ Nanyi watu weusi wapendwa, huko Kusini, jinsi mliyopiga kura! Mnasema, “Huna shughuli yo yote kusema hayo mimbarani,” Loo, ndio, ninayo, ni Neno la Mungu! Na doa la—la Abraham Lincoln, yule aliyewaweka huru, likiwa kwenye jumba la makumbusho kwenye nguo ya mwanamke, nanyi mnauza haki yenu ya mzaliwa wa kwanza. Hamna aibu.

⁶⁸ Nanyi watu, kwa ajili ya siasa, ati kwa sababu tu ninyi ni Wanademokrati wazuri, mlipigia kura kitu kama hicho; na

mkauza haki yenu ya mzaliwa wa kwanza ya Umarekani na Ukristo, mkampa yule kahaba aliyetufukuza tukaja kwenye nchi hii, kile kilichotufanya jinsi tulivyokuwa. Mnaona jinsi alivyokuwa akinyemelea na kuingia ndani? Kwa urahisi sana, mpaka hivi sasa amekalia kiti cha enzi. Hakika! Kiti cha enzi cha Ikulu ya Marekani.

⁶⁹ Angalia! Tayari... Je! mliona hivi majuzi kuhusu shule za Kikatoliki na shule za Kiprotestanti? Kusaidia shule ya Kikatoliki lakini si ya Kiprotestanti. Unaona? Loo, ndugu! Sasa angalieni wimbi la uchafu likija sasa. Angalia, nao kama walivyofanya jambo hilo, angalia kilichotukia. Dhambi hii yote ikilundikana. Imefikia mahali fulani na imeliweka taifa katika hali hiyo ya kuyumbayumba.

⁷⁰ Miaka michache iliyopita, wakati walipokuwa na... Wapentekoste walipojitenga kwa mara ya kwanza, jambo hilo liliokoa taifa miaka michache iliyopita wakati Al Smith alipokuwa akitaka kupigiwa kura. Marekani ilipambanua vyema wakati huo. Lakini Pentekoste ikawa ya kimwili sana ikaendelea moja kwa moja na kuingia kuuza haki zao kama Mkristo, kwa siasa, na ni siasa mbele ya Biblia. Loo, jamani!

⁷¹ Sasa, hebu kidogo, na hebu ona jinsi jambo hili linavyotokea. Sasa, tunaona waliyofanya na mambo waliyofanya, tunayaona yakienda sambamba kabisa hapa, dhambi kila mahali. Yezebeli aliingia, akawaroga watu wote. Na tazama, hatimaye, akaanza kumjengea Balaamu madhabahu kubwa. Hiyo ni kweli? Nao makuhani wa Balaamu wakakusanyika kutoka kila upande wapate kuingia mahali pale, na kuanza kuinajisi nchi kwa ibada za Balaamu.

⁷² Angalia jinsi walivyofanya, angalia jinsi walivyojiingiza ndani. Mambo tu ambayo wamefanya, angalia walipo leo. Angalia Ukatoliki ukimeza, ukimeza, ukimeza; ukiungana, ukivunja kitu hiki, jinsi hasa Danieli alivyosema wangepanya. Chuma na udongo havitachanganyika, bali watachanganya mbegu zao wao kwa wao, wakivunja. Kila msichana wa Kiprotestanti anayeolewa na mvulana wa Kikatoliki hana budi kuwalea watoto wake wawe Wakatoliki. Yote namna hiyo, kuoana, kuchanganyikana, namna hiyo mpaka imefikia mahali ambapo Marekani nzima imeingiliwa kila mahali.

⁷³ Tutafanya nini kama wamishenari, tukitoka kwenda kukomboa huko Marekani ya Kusini na kila mahali sehemu hiyo ya ulimwengu, Tommy Osborn na hao wengine, wakijaribu kuwatoa watu kutoka kwenye upagani huo nao wanaweza kuelekeza kidole chao moja kwa moja huko nyuma ya kwamba tulimchagua kiongozi wetu, na jambo lile lile. I—itakuwaje kwa ulimwengu huu? Linapaswa kumtikisa kila mtu aliyepo hapa ndani. Tutajibuje? Mmishenari atasema nini wakati wao wanasema, "Mlikuja hapa kutukomboa kutokana na kitu hiki,

na watu wenu wenyewe wameweka kitu kile kile ofisini mwenu kule, kwenye kiti cha enzi”? Tutaninii- . . . Nini . . .

⁷⁴ Angalia nyuma katika kurasa za historia, geuka uone kama—kama si kinyume kabisa, karibu, cha katiba kufanya hivyo. Wasingefanya jambo hilo miaka kadha iliyopita lakini, unaona, tumeuza haki zetu za Kikristo kwa siasa, na hivyo ndivyo Ibilisi anavyojipenyeza mwenyewe ndani. Ahabu hakuwa kitu ila kibaraka wa Yezebeli. Hivyo ndivyo tu huyu atakavyokuwa, kibaraka tu. Hatafanya hivyo yeye mwenyewe, lakini mfumo huo ulio nyuma yake utamfanya afanye hivyo. Kweli kabisa! Finya dhamira yako, ewe Mkristo. Jitikise, wakati umeendelea sana kuliko unavyodhania. Hali tuliyomo, hali waliyokuwamo, na jinsi walivyojiachilia wakalegea.

⁷⁵ Jinsi ambavyo hapana budi ule moyo mkuu wa Mungu wenye upendo ulilia sana, na kuomboleza, alipowaona wamishenari Wake. Akawafanya mfano, mataifa yote yakija kila mahali kwa sababu Mungu alikuwa amewabariki, akiwaona katika umoja. Kiroho, wakimtumikia Mungu. Na halafu kuwazia ya kwamba Yeye—Yeye alitamani kuwaona wakirudia upendo wao wa kwanza na kufanya yaliyo haki, bali daima walitokomea, na kuondoka, na kutokomea, mpaka hatimaye Yezebeli akaingia. Hivyo ndivyo tulivyofanya hasa. Tumepeperuka kutoka kwenye kanuni za Kristo. Wakati Mungu alipowatuma wahudumu wake kote nchini, walihubiri utakatifu, Wapilgrim Holiness, Wanazarayo, Wapentekoste, “Mrudieni Mungu! Mrudieni Mungu!”

⁷⁶ Na yale makanisa kweli kweli ya zamani yaliyoiimarika yalicheka tu na kufanya mzaha. Wengi wa hao waamini wa kisasa, mbona, walikataa kabisa kila kitu ambacho hao watu walifanya na kusema “Ilikuwa ni cha Ibilisi.” Ilifanya nini? Na kanisa likaanza kusikiliza jambo hilo, walio wengi wakaanza kusikiliza. Muda si muda, unajua, kama mwanamke Mkatoliki angeweza kuvaa vitu kama hivi, Mprotestanti angeweza pia. Kama kanisa Katoliki liliweza kufanya hili, la Kiprotestanti lingeweza pia. Ndipo kama Mmethodisti angeweza, na Mbatisti je? Ndipo kama Mbatisti angeweza, na Wapentekoste je?”

⁷⁷ Unaona, huko ndiko mifumo ya kujibunia inakokuingiza. Haleluya. Hiyo ni kweli. Hiyo ndiyo sababu ninapinga mifumo hiyo, kwa maana Neno la Mungu linaipinga. Mfumo wa kujibunia: Mungu anaupinga, Neno Lake linaupinga, manabii Wake wataupinga, watumishi Wake wa kweli wataupinga, wote waliozaliwa na Roho wa Mungu wataupinga.

⁷⁸ Angalia jinsi Israeli ilivyofanya, jinsi walivyochukuliwa na mawimbi, hata hatimaye Yezebeli akaja. Angalia jinsi Marekani ilivyofanya, na kuchukuliwa na mawimbi ya kilimwengu, mpaka hatimaye Yezebeli akachukua kiti cha enzi. Hiyo ni kweli. Sasa, Yezebeli kwa kweli hakuwa kwenye kiti cha enzi cha Misri . . .

kiti cha enzi cha Israeli, lakini ndiye aliyekuwa kiongozi mkuu nyuma ya kiti cha enzi. Na serikali ya kidini ya Kikatoliki haimo kwenye kiti cha enzi cha Marekani, lakini hilo ndilo mfumo ulio nyuma yake kwa sababu imeungana naye. Na Biblia ilisema, katika nchi hii, watafanya “sanamu *inayofanana na yule mnyama*.”

⁷⁹ Loo, ndugu, dada, kuna nini? Vema, na—najua ni kitu gani. Biblia ilisema wangeuteka wakati huu wa Laodikia, na hapo ndipo tulipo. Huenda mkanichukia sasa, bali siku moja hamtanichukia wakati mtakapojua Kweli ni nini. Huenda usikubaliane nami na uinuke na kutoka kwa vishindo humu jengoni, hilo linaonesha tu ujinga wako. Lakini siku moja utatambua, siku moja utatamani na kujua ya kwamba ni Kweli! Ninanena Hilo katika Jina la Bwana! Ninajiweka kama mlengwa, jambo ambalo hatimaye litanipeleka kaburini. Nitakuwa shahidi mpaka nife, kama Mungu atanisaidia. Hiyo ni kweli.

⁸⁰ Tuko hapa katika hali hii, tuliyomo siku hizi, yote yakiendelea namna hiyo. Na Israeli, jinsi Ahabu alivyofanya, kibaraka kwa Yezebeli maana alikuwa—alikuwa amemuoa yeye. Marekani, kiongozi wetu, ilikuwaje... Mnajua kiongozi wetu alikuwa ni tajiri? Ni wangapi wanaojua jambo hilo? Milionea tajiri sana. Mtu fulani aliniambia, katika gazeti fulani ama radio fulani ama televisheni ama kitu kama hicho, Jack Benny ama mtu fulani alininii... Ernie Ford, nafikiri ilikuwa ndiye. Mtu fulani alisema ya kwamba “Baba yake alimsaidia kupata mikoa miwili ambayo haikuwa yake.” Karibu anamiliki hiyo mingine. Aliipataje? Pesa hizo zilitoka wapi? Kupitia kwenye biashara ya wiski, na pombe. Hiyo ndiyo sababu alipunguza kodi ya wiski na kadhalika. Hicho ndicho kilichomtajirisha. Kitu kile kile kabisa kilichotea laana nchi yetu, kitu kile kile hasa kilichopotosha akili za watu wetu, kitu kile kilichowapeleka vijana wetu kuwa walevi, na wasichana wetu kuwa malaya, pesa zilizotokana na kitu hicho zilimtajirisha.

⁸¹ Kitu kile kile, ule mfumo wa kale wa Yezebeli, kitu kile kile kilichowatesa watu wetu, kitu kile kile kilichowalevy (katika Urumi) na kuwachoma moto na kuwapasua katikati na kuwafanyia kila kitu, damu ile ile ya wafiaimani (Biblia inasema) imo ndani yake! Hao hapo, wamefunga ndoa. Na sisi Wamarekani tunaendelea kuyumbayumba moja kwa moja, “Loo, vema, tuna dola chache za ziada nasi tuna wakati wa raha. Sisi ni matajiri kuliko mataifa mengine.” Lakini, ndugu, hebu ngoja kidogo.

⁸² Hebu na tulichunguze kwa makini sana sasa, kwa dakika chache zifuatazo, tuone ilivyotukia.

⁸³ Wahubiri waliendelea moja kwa moja na kupatana nao, wakaenda moja kwa moja pamoja nao, mfumo huo mzima.

Mfumo wote wa Israeli uliambatana moja kwa moja na Yezebeli. Walikuwa na mfano, naam. Na je! Biblia haitwambii ya kwamba katika siku hizi za mwisho tutakuwa na “mfano ya utauwa”? Unabii wote umetimizwa, ndugu, tuko katika wakati wa mwisho! Kitaifa, tuko katika wakati wa mwisho! Kiroho, tuko katika wakati wa mwisho! Kila mfumo uko katika wakati wa wake wa mwisho! Jambo linalofuata ni kuja kwa Bwana na kuhamishwa kwa Kanisa.

⁸⁴ Mungu alituma kila ishara, ajabu, alifanya kila kitu alichoweza kufanya, akijaribu kuwavuta watu, na daima wakaingia moja kwa moja. Angalia mji huu hapa, angalia nchi hii hapa, ikiwa na makumi ya mamia na mamia ya Wapentekoste; na kwa sababu ya kuitetea Kweli, wako wapi alasiri ya leo? Kwa kuwa mtu fulani aliwaambia wasishiriki katika mkutano huu. Enyi maskini, ninii . . . Mungu na awarehemu, ndilo ninaloweza tu kusema. Wakati ninyi Wakristo mkiwa hamna uti wa mgongo zaidi ya huo, mna mfupa wa kuku badala ya uti wa mgongo. Kweli! Tunachohitaji ni “kuhubiri Injili iliyo na meno,” ambayo itakatakata kitu hicho vipande-vipande. Mlienda kama tu wengine wao, ndipo mnashangaa kwa nini tunalipigia makelele jambo hilo. Ndipo, unaona, mnakuwa na “dharau.” Ninatarajia jambo hilo, sina budi kutarajia.

⁸⁵ Mambo hayo yote yaliendelea huko Israeli. Hatimaye, siku moja, mtu mmoja mzee mwenye mwili ulio na nywele nyingi, akaja kutoka nyikani, akitembea kwa kishindo, Eliya Mtishbi. Yeye hakutoka kamwe katika madhehebu yo yote, alitokea nyikani! Hakuwa na uhusiano wo wote nao. Alikuwa ni nabii wa Bwana. Ndugu, yeye alitikisa ufalme huo wa Yezebeli kwa kila kitu kilichokuwa humo. Walimchukia. Hakuungwa mkono, nitawahakikishieni jambo hilo. Biblia inasema hakuungwa. Kweli. Aliwafanya hao akina Yezebeli waliojipaka rangi “waghadhabike,” nadhani. Aliweka shoka kwenye shina la mti kama Yohana alivyofanya, vipande viliangukia po pote vilipotaka, lakini alimweka pale. Alilitikisa taifa hilo, akiwaonesha ya kwamba walikuwa wamekosea, na akijaribu kuwarudisha kwa Mungu wa kweli aliye hai, na kwenye Neno Lake badala ya kumwabudu Yezebeli.

⁸⁶ Wao walifanya nini? Je! walimpokea? Walimchukia! Lakini Neno lake lilisonga mbele vivyo hivyo, kwa sababu yeye alikuwa na BWANA ASEMA HIVI! Mungu alitenda kazi pamoja naye, na akaonesha alikuwa ni nabii aliyetiwa mafuta kwa kutimia kwa mambo aliyosema. Na yote aliyofanya yalithibitisha ya kwamba yeye alikuwa ni nabii wa Mungu. Lakini hata hivyo hawangeamini jambo Hilo, kwa sababu yeye alivunjilia mbali manyumba yao ya michezo ya kuigiza. Aliwaambia ya kwamba walikuwa “Wamekosea!” Ahabu alikuwa ni kibaraka. Kweli! Na unaona hawakumwamini, bali alihubiri jambo Hilo hata hivyo. Hakuna hata mmoja wa wahubri aliyekubaliana naye,

yeye alisema, “Mimi ndimi pekee niliyesalia, Bwana. Waangalie, hata hawataninii. . . kwanza, hakuna mtu anayeniunga mkono.” Lakini yeye alikuwa na kazi ya kufanya na aliifanya. Alikuwa na Neno la Bwana, BWANA ASEMA HIVI! Naye alishambulia taifa hilo, akashambulia kanisa, akashambulia kila kitu kilichokuwako, na Mungu alikuwa pamoja naye!

⁸⁷ Tumeahidiwa, katika siku za mwisho, ya kwamba yeye atarudi katika nchi hii pia. Ninajua, Yesu, wakati. . . Mathayo 17, wakati walipomwuliza, “Kwa nini Waandishi hunena, ‘Eliya. . .?’”

⁸⁸ Angalia kile Yeye alichosema, “Eliya kweli hana budi kuja kwanza,” wakati uliopita, wakati ulio- . . . wakati, ujao, lakini basi akamtoa Yohana kama mfano. Yohana hakuwa Malaki 4. Yohana alikuwa ni Malaki 3, “Tazama, ninawapelekea mjumbe mbele Zangu, kuitengeneza njia.”

⁸⁹ Malaki 4, Yeye alisema:

Kabla haijaja siku ya Bwana iliyo kuu na ya kuogofya, wakati ulimwengu wote utakapoteketezwa kama makapi; kabla ya siku hiyo, nitampeleka Eliya.

⁹⁰ Na haikuwa Yohana, kwa sababu Bwana kamwe hakuiteketeza nchi wakati Yohana alipokuja. Na kama ukiangalia, na katika ule mlango wa mwisho, katika kile kifungu cha mwisho, Yeye alisema, “Naye (angalia; yeye, akizungumza. . .) ataigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto wao, na mioyo ya watoto iwaelekee baba zao.”

⁹¹ Sasa angalia! Yohana wa kwanza alikuja, Eliya wa kwanza, yeye alifanya nini? Alikuwa na akaleta Ujumbe na kuigeuza mioyo migumu ya imani ya mababa wa kale ielekee imani ya kanisa hilo changa, hao watoto. Bali wakati Eliya huyo mwingine alipokuja, katika wakati wa mwisho, yeye anapaswa kurudi nyuma na kuichukua mioyo ya ba—baba. . . mioyo ya watoto, hasa, na kuigeuza iirudie Imani ya baba wa kipentekoste. Unaona tofauti yake? Yeye hatakuwa mmoja wa hawa *wanaojiita* tulio nao siku hizi, yeye atarudi moja kwa moja kwenye Matendo 2 na kuanzia moja kwa moja kutoka hapo. Atahubiri Injili isiyoghoshiwa, atanena tu mambo yale ambayo Petro alinena kwenye Siku ya Pentekoste, maana yale aliyosema kwenye Pentekoste yamethibitisha Maandiko mengine yote. Yeye hatajifunga na madhehebu fulani, wakati Eliya atakapokuja. Atawachukia wanawake kama Eliya alivyofanya, kama vile tu. . . ama wanawake wabaya, kama vile tu Yohana alivyofanya. Atapenda kukaa nyikani kama wao walivyokuwa. Hatahurumia. Tunamtazamia aje. Atakuja! Mungu alisema atakuja, naye atawasili!

⁹² Ninaamini, kwa vyo vyote, Ujumbe tulio nao leo utakutangulia kule kuja kwake kukuu. Naam, bwana! Yeye yuko njiani, amezaliwa tayari. Kama vile Eliya alivyokuwa,

naye akipasua kutoka nyikani, atajitambulisha mahali fulani. Atahuribi Matendo 2. Atairudisha Imani ya hawa baba wa kale wa kipentekoste irudi moja kwa moja kwenye... imani ya hawa watoto wa kipentekoste, iirudie Imani ya baba wa kipentekoste. Atarudi moja kwa moja kwenye Matendo 2, Matendo 2:38, kuanzia kote huko nyuma. Ataleta Injili halisi, isiyoghoshiwa. Hatakuwa na uhusiano wo wote na Yezebeli na mfumo wake. Atakuwa ni mtumishi wa Mungu. Hakika! Biblia ilisema yeye atakuja. Atatoa unabii na kulipua Ujumbe wake mbele ya hawa Mayezebeli, jinsi ile ile tu kama Eliya alivyofanya hapo mwanzo kwa Israeli. Wao watamchukia! Hawatashirikiana naye, la. Yeye atakuja! Mungu aliahidi jambo hilo, naye atajitokeza jukwaani. Ata—atalihubiria Kanisa lililoteuliwa kama ilivyonenwa atafanya, akiwatikisa hao Wateule, akitikisa na kuondolea mbali mambo ya kimwili, u—ulimwengu na kadhalika, akiyatikisa yaanguke, akiyachemsha kabisa, na akilikusanya Kanisa pamoja, watu fulani.

⁹³ Ninajua mnasema, “Hayo ni madhehebu yangu.” Ndugu, umekosea! Yohana alikuja kama mfumo wa mtu mmoja kumtambulisha Mtu fulani Mmoja: Yesu Kristo. Wala Eliya hatakuwa ni mfumo fulani, itakuwa ni mtu mmoja, Yesu alisema hivyo. Itakuwa ni mtu mmoja aliyetiwa mafuta na Roho Mtakatifu. Wala yeye hataleta miungu mitatu ama minne, atamtambulisha Mmoja: Bwana Yesu Kristo, maana Ujumbe wake utawatikisa watoto wa kipentekoste kuirudia Imani ya baba zao tena.

⁹⁴ Kumbuka, ndugu, kama ninasema mambo haya kusudi nichukize, ninapaswa kuwa madhabahuni. Ninawaambia BWANA ASEMA HIVI! Kama Mungu hajathibitisha nimewaambia Kweli, kote nchini, kote ulimwenguni, basi niambieni makosa yalikuwa wapi. Ninawaambieni Kweli! Mrudieni Mungu, upesi! Tokeni kwenye madhehebu haya, maana Biblia inasema, katika Kitabu cha Ufunuo, ya kwamba, “serikali Katoliki ya Kirumi ilikuwa ni kahaba, naye alikuwa ni mama wa makahaba.” Hiyo ni nini? makanisa, mifumo.

⁹⁵ Hivi kanisa la Kimethodisti, kanisa la Kiluteri, yalitoka wapi? Kanisa la Kimethodisti, Kibatisti, madhehebu yote yalitoka wapi? Mungu kamwe hajafanya kanisa kuwa madhehebu. Kanisa Katoliki walisema wao walianzia kule nyuma, “Yesu alipounda madhehebu ya kanisa.” Na—nataka ukurasa katika historia, ama ukurasa mmoja katika Biblia. Kamwe hapajatokea madhehebu kwa miaka mia tatu na na sita, baada ya kifo cha mtume wa mwisho, ndipo wakaunda Baraza la Nikea na kuunda madhehebu. Na wakati Luther alipotokea... yeye alikuwa ni mtu mashuhari wa Mungu, bali mara tu yeye alipoondoka, kundi hilo dogo la watu liliondoka na likaenda kuunda madhehebu mengine. Ndipo Roho Mtakatifu akatoka akashuka juu ya John Wesley, yeye kamwe hakuunda

madhehebu yo yote, bali baada ya kuondoka kwake ndipo wao wakaunda madhehebu. Ndipo Roho Mtakatifu akaja na Wapentekoste, nao wakatoka kwa Methodisti. Halafu ni jambo gani lililotukia? Ndipo *wao* wakaunda madhehebu.

⁹⁶ Lakini kutakuwa na mfumo wa mtu mmoja utakaokuja kwa nguvu na upako wa Eliya, kutimiza unabii huu. Haleluya! Yeye atatikisa kitu hicho. Na, kumbukeni, yeye aliwatabiria, na kutabiri, na kuwaambia mambo yote, na Mungu akatenda kazi pamoja naye. Lakini Ujumbe wake wa mwisho ulishambulia Ikulu. A-ha. Wakati Yohana alipokuja, Ujumbe wake wa mwisho ulikuwa ni wa kushambulia Ikulu ya wakati huo. Ujumbe wa mwisho wa Eliya, wakati aliposhuka kwenda kwenye barabara hiyo asubuhi hiyo baada ya kuwa katika Uwepo wa Mungu kule nje, akashuka kwenye barabara hiyo na mvi zikitokea kila mahali mwilini, kichwa chake chenye upara kiking'ara, masharubu yakipepea, maskini macho hayo mazee, yakimetameta kwa utukufu wa Mungu. Fimbo ile mkononi mwake, na miguu yake ikiwa imara tu ilivyoweza kuwa. Alikuwa anafanya nini? Akishuka moja kwa moja kutoka Samaria kwenda mbele ya Ikulu, na kusema, "BWANA ASEMA HIVI!" Pasipo kuogopa lo lote. Makanisa yalikuwa yamempuuzwa, watu walikuwa wamempuuzwa, kwa hiyo sasa yeye anafanya shambulizi lake la mwisho, juu ya Ikulu.

⁹⁷ Basi ni jambo gani lililotukia baada ya hayo? Sikilizeni! Baada ya shambulizi hilo, sauti yake ilinyamaza, hakuna mtu aliyemsikia tena. Mungu alimwita akatoke jukwaani, kasema, "Eliya, tayari umeutangaza Ujumbe wako kwa Israeli nzima, wanaujua. Sasa njoo huku nyikani, waache, jitenge nao maana nitafanya jambo fulani. Nitawaonesha maana ya kuukataa Ujumbe Wangu." Ni nini kilichotokea? Vita, njaa, ukosefu wa chakula.

⁹⁸ ROHO MTAKATIFU ASEMA HIVI, "Angalieni kwa makini yale yanayokuja! Angalieni kitakachofuata! Kulikuwa na njaa, Kutakuwa na njaa!" Loo, labda si ya chakula, bali ya kulisikia Neno la Mungu na Kweli Yake. Makanisa yote yatafungamana na kuingia moja kwa moja kwenye jambo hilo jinsi ile ile, kama tu vile walivyokwisha kumezwa na jambo hilo.

⁹⁹ Eliya alifanya nini? Aliona kijito kilichofichwa, huko juu sana mlimani ambako alipata Maji ya Uzima, mafunuo ya Kiungu kutoka kwa Mungu alipokuwa anaketi kule chini ya nguvu za Mungu. Mafunuo hayo yakiwa ni kijito kidogo kilichofichwa, wakati hao wengine walipokuwa wanataabika kwa njaa. Na Mungu na akawabariki watumishi Wake (hao kunguru), walimletea chakula wakati alipokuwa ametengwa na watu. Nao walikuwa kule wakionea njaa ufufuo na kila kitu kikiendelea, "Msisikilize tena ufufuo wake hata... Yuko wapi yule mzee mwenda wazimu anayeenda akiyalipua madhehebu yetu? Yuko wapi sasa?" Hawakujua. Yeye alifanya uhusiano

wa karibu zaidi na Mungu, huko mahali palipotengwa ambako hawakusikia sauti yake. Ndipo wakaanza kuona.

¹⁰⁰ Wakati Mungu anapotuma Ujumbe na kuwaambia watu, nao hawaupokei, ndipo Yeye humwondoa mtumishi Wake kisha anatuma mapigo Yake: njaa, mauti (tukinena kiroho, kimwili pia). Hebu ngojeeni majonzi, ndugu. Mnadhani mmeona kitu cho chote, ninyi subirini tu baada ya kitambo kidogo. Hamjaona kitu. Mnadhani mnakufa kwa kuuokosa ufufuo mzuri wa kiroho, ninyi, ngojeni mpaka baada ya kufikia kitambo kidogo. Ninyi subirini tu, mtatamani na kulia kwa kukosa kulisikia Neno la Mungu. Biblia ilisema hivyo! “Kutakuwako na njaa katika siku za mwisho,” alisema nabii, “wala si ya chakula na maji peke yake, bali ni ya kulisikia Neno la kweli la Mungu.” Sauti hiyo itanyamaza, nyikani mahali fulani, imefichwa.

¹⁰¹ Yeye aliwaamuru kunguru, watumishi Wake. Hao ndege na wabarikiwe, watumishi Wake, walioidumisha sauti ya—ya Eliya kuwa hai katika wakati wa kutengwa kwa—kwake na kanisa. Kunguru walimletea nyama na mkate asubuhi, na nyama na mkate jioni, naye akanywea chemchemi ndogo wakati hao wengine huko chini walikuwa hawana chakula chote chote cha kiroho wala maji ya kiroho.

¹⁰² Ndipo siku moja, baada ya dhambi kuenea sana, naye Mungu alikuwa amewafanya watu Wake watubu. . . Yezebeli alichukua kila kitu, alisafisha kila kitu, naye atafanya jambo hilo tena! Hiyo ni BIBLIA TAKATIFU YA MUNGU INASEMA HIVI, “Atafanya jambo hilo tena.” Yeye yuko moja kwa moja kwenye kiti cha enzi sasa, nyuma ya yule kibaraka; akimwelekeza kwenye njia yo yote atakayo, hakuna mtu atakayemzuia. Bila shaka, hakuna atakayemzuilia sasa, kwa sababu kile ambacho wasingeweza kupata katika makundi ya kidini wamepata—wamekipata chote kwenye siasa, na hapo wakafanya jambo hilo. A-ha, hivyo ndivyo walivyofanya hasa. Ambapo, siasa zitakuwa ni kususia moja kwa moja kurudi kwenye ile alama ya mnyama, kwa hakika kama ninavyosimama hapa, unaona, kama Biblia ilivyosema.

¹⁰³ Ninajua tunachelewa, nitaharakisha. Sina budi kuingiza neno hili la mwisho ndani, Bwana akiniruhusu.

¹⁰⁴ Angalia! Eliya alikaa kule mpaka Mungu alipomtuma. Hakuwa na ufufuo. Hakuhubiri dhidi ya cho chote kile. Yeye alisimama kule tu peke yake pamoja na Mungu, huko nyikani, maana yeye alikuwa ni mtu wa nyikani. Alilelewa nyikani. Vivyo hivyo na Yohana alilelewa nyikani.

¹⁰⁵ Alitoka akaenda huko nyikani peke yake pamoja na Mungu, akaondoka kanisani baada ya kutoa Ujumbe wake. Nalo kanisa likaukataa, liliukataa. Na hatimaye madhehebu hayangefanya cho chote, kwa hiyo ilimbidi tu kutoka kwenda zake. Mungu alimwondoa kwenye jukwaa, akamchukua akampleleka huko

nje nyikani, kasema, “Njoo huku, hao hawatasikiliza tena. Njoo, ndipo nitawashushia hukumu Yangu.” Loo, ndio, yeye atakuwa hapa moja ya siku hizi, wewe ngojea.

¹⁰⁶ Ndipo, baada ya siku za unabii wake, ilikuwaje? Kanisa lilidhoofika, lile tisho kuu la Yezebeli, aliwachukua wote kwake, akawameza wote. Akawachukua kwake, na kujenga maashera na cho chote kile.

¹⁰⁷ Lakini, siku moja, Mungu alimwita atoke tena! Huyu hapa akatoka. Sikilizeni kwa makini sasa, na msinikasirikie. Mimi ninasema, “BWANA ASEMA HIVI!” Wakati alipotoka, Mungu alifanya nini? Alimtuma kwa mwanamke mjane. Wakati mmoja huyo mwanamke alikuwa na mamlaka ya mwa—mwanamume juu ya kichwa chake, bali ilihitajika mauti kumweka mwanamke huyo huru kusudi apate kuamini Neno la huyo nabii. Unaona jambo hilo? Yeye alikuwa na mume aliyemwongoza kwenda hivi na vile, kwenye moja ya shule kule chini. Lakini wakati wa ukame huu mkuu, mwanamume huyo alikuwa amemezwa, mauti ilikuwa imemtwa. Huyu mwanamke hakuwa amefungiwa tena kwenye madhehebu yo yote, kwa hiyo alikuwa tayari sasa kusikia Neno la Bwana. Mwanamke, ikimaanisha Kanisa; mjane, ambaye mumewe (madhehebu) alikuwa amekufa, naye mwenyewe alikuwa tu akiwazia alikuwa anaishi kwa shida kabisa. Ndipo Mungu akasema, “Shuka uende kwake sasa, atakusikia, nimemwagiza.”

¹⁰⁸ Loo, tunafikiria wakati mwingine, ninyi kundi dogo pale ambalo ni aminifu sana na mnafanya lo lote mwezalo kuwa na mkutano, kujaribu kuwaonesha watu ya kwamba moyo wenu uko sawa nanyi mnawataka wawe sawa, mnafikiri mnaishi maisha magumu. Lakini, kumbukeni, Mungu ameelekeza jicho Lake kwenu! Mnampenda, ninajua mnampenda, hamngeketi hapa, hamngehudhuria kitu cho chote kama hicho. Mungu ameelekeza jicho Lake juu yenu. Naam!

¹⁰⁹ Na wakati alipofanya jambo hilo, mumewe alikuwa amekufa, madhehebu yake yamekufa, kwa hiyo sasa yeye yuko tayari kusikia Neno la Nabii. Kwa hiyo wakati nabii alipokuja kwenye lango na kumwomba ma—maji kidogo anywe, aliondoka akaenda kuyaleta. Ndipo akasema, “Niletee mkate kidogo.”

¹¹⁰ Ndipo akageuka akasema, “Kama Bwana aishivyo, sina kitu ila cha kutosha tu.”

¹¹¹ Sasa, ilionekana kana kwamba alikuwa ametumwa kuchukua cho chote kidogo alichokuwa nacho, bali ilikuwa ni vinginevyo. Wakati alipokuwa tayari kutoa alichokuwa nacho kuunga mkono Neno, Mungu alimlisha. Na endapo uko tayari kutoa Roho uliyo nayo, Roho ambayo Mungu amekupa kuunga mkono Neno, basi Mungu atakuweka hai. Haleluya! Naam, Mungu atukuzwe! Je! mnaona jambo hilo, enyi kanisa? Msifikiri nimerukwa na akili, la. Lakini cho chote ulicho nacho, kiasi

kidogo unachomwamini Mungu nacho, imani yo yote uliyo nayo, iweke kwenye Neno, si kwenye madhehebu! Iweke kwenye Neno la Mungu, Yeye atakufanya hai.

¹¹² Alikuwa tayari wakati huo, maana asingekuwa hapo nyuma, maana wasingemruhusu. Lakini sasa yuko tayari. Je! Atapokea? Mungu alimtuma nabii kwake. Je! atapokea Neno lake? Atampokea nabii huyu? Naam, alimpokea. Naye akamwambia, akasema, “Sasa, uhai mdogo wo wote ulio nao, uweke hapa ndani, niletee kwanza.” Na ni jambo gani lililotukia? Wakati watu wengine wote walikuwa wakiteseka na kufa kwa njaa, yeye na watoto wake na nyumba yake wote walikula chakula kizuri mara tatu kwa siku, Ufunuo wa kiungu wa Neno. Ninatumaini unalipata, ewe rafiki.

¹¹³ Ni jambo gani lililoendelea? Alikaa pale pale mpaka njaa ilipokwisha, akikaa na mwanamke huyu (Kanisa hili) lililompokea na kuamini Neno Lake. Naye akamwezesha kuwa hai (akaliwezesha Kanisa kuwa hai) kwa Neno la Bwana, kwa sababu alisema “BWANA ASEMA HIVI.”

¹¹⁴ Sasa, hatuna wakati wa kumalizia hadithi iliyosalia, unajua, jinsi ilivyombidi kufikia shindano la kuamua na Baali. Atafanya jambo hilo, moja ya siku hizi, msijali. Atakapokuja kishujaa kutoka nyikani, angalia jambo litakalotukia.

¹¹⁵ Nini kilitukia? Ndipo wakati maskini mzee mwema Eliya, yule nabii, mtumishi halisi wa Mungu, alipofikia mwisho wa safari yake, Mungu alimwambia, siku moja, kasema, “Eliya, umehubiri muda mrefu vya kutosha sasa. Umepigana na Yezebeli na rangi yake yote na kila kitu mpaka ukakinaiwa.” Kasema, “Shuka uje Yordani!” Naye huyu hapa anaenda, akafika Yordani. Hapo kile kijito cha kale chenye matope kikitiririka kule, chenye maji baridi sana, ya barafu, jambo ambalo itambidi kila mwanadamu kukabiliana nalo: Yordani, mauti.

¹¹⁶ Lakini wakati mtumishi huyu mkuu wa Mungu aliposhuka kwenda Yordani, na mwanawe akitembea pamoja naye, mwana wa Injili, ...Loo, naam, yeye alikuwa ni mwanawe, “Baba yangu, baba yangu, magari ya Israeli, na farasi wake.” Wakati yeye na mwanawe walipotembea wameshikana mikono, kwenda Yordani, alikuwa akimwambia babaye akiondoka asubuhi hiyo.

¹¹⁷ Wakati alipofika Yordani, alinyosha mkono wake na kutwaa lile joho la nguvu kutoka mabegani mwake, akasema, “Mauti, huwezi kunifanyia jambo lo lote.” Naye akaupiga Yordani, “Ondoka, ninavuka asubuhi ya leo.” Ni jambo gani lililotukia? Ulirudi nyuma na kukauka kama vumbi. Maskini yule nabii alikuwa akifanya nini? Alikuwa akiangalia ng'ambo ya Yordani, alijua kulikuwa na gari lililokuwa linamngojea kule pamoja na farasi zake. Alikuwa anaenda nyumbani,

kazi yake ilikuwa imekwisha. Mwanawe katika Injili alikuwa akipachukua mahali pake.

¹¹⁸ Nilikuwa nikija nyumbani hivi majuzi kutoka huko Magharibi. Ninakumbuka jambo hili. Nilifungulia redio (ilinibidi kuendesha gari kwa siku tatu, maili elfu mbili mia nne, peke yangu). Nikafungulia redio yangu na ni-... nikisikiliza nyimbo za kiroho kutoka kwa Del Rio, Texas. Kulikuwa na mtu aliyezungumza juu ya mzee mmoja mnegro, mweusi. Alikuwa anakaribia kufa na ilibidi ashuke kwenda mtoni, akasema, “Hizo ndara za dhahabu nitakazovaa, kutembea kwenye barabara za dhahabu.” Maskini mzee huyu wa kinegro alikuwa amehubiri maishani mwake mwote na jambo pekee aliloweza kufikiria lilikuwa ni kustarehe, yote aliyokuwa nayo, ilikuwa ni gambusi lake la zamaini lililoning’inia ukutani. Aliketi juu ya robota za pamba na kuimba zile nyimbo, alijipumzisha kutoka kwenye huduma yake, na gambusi hilo la kale. Hiyo ndiyo njia aliyokuwa nayo, ya kujipumzisha. Alisema yule farasi mwenye mkia mfupi aliyekuwa akimpanda atakuwa kule chini pamoja na gari lake. Nilikuwa nikiwazia habari zao. Akasema, “Hizo ndara za dhahabu nitakazovaa, kutembea kwenye barabara za dhahabu.”

¹¹⁹ Na alipomaliza kuimba, nikaifunga redio. Nami nilikuwa nikienda kule, nikishika usukani, “Loo, hiyo ni kweli. Ninajua ni kweli, sina budi kushuka kwenda kule pia. Ni kitu gani kilichonifariji daima? Nitapata wapi faraja yangu nyikani?” Nina maskini bunduki ndogo inayoitwa... Ninawinda nayo majira ya kupukutika majani. Ni ya .270, mtindo wa 721, Remington. Mtu fulani, ndugu, alinipa, huko California, miaka kadha iliyopita. Nimewinda nayo kwa miaka kadha wa kadha. Jinsi... jinsi imekuwa ni faraja, maana na—najua ni bunduki nzuri ya kuwindia, ndiyo faraja yangu huko nyikani.

¹²⁰ Ndipo nikawazia juu ya ono langu. Nilipofika kule na kuwaona watu wangu wote, nilisikia kitu fulani kikilialia, na huyu hapa maskini Prince wangu anakuja (maskini farasi wangu wa kusafiria) na kuweka kichwa chake juu ya bega langu. Nikawazia, “Naam, moja ya asubuhi hizi ninashuka pia, kwenda Yordani.” Na maskini .270 niliyokuwa nikinini... inaning’inia ukutani. Sijaitoa tangu siku nyingi, mwishoni mwa mwaka jana. “Maskini farasi yule wa kusafiria niliyekuwa nikimpanda, Mungu atakuwa amemfungia kwenye gari langu, kwenye asubuhi hiyo nitakaposhuka kuja mtoni.” Atakuwa amesimama upande wa pili tu wa mto kule. Mungu atamtuma, nilimwona hivi majuzi usiku. Atafungiwa kwenye gari langu, moja ya asubuhi hizi. Nitakuwa nimeondoka, nikipanda kupitia mawinguni.

Na tuombe.

¹²¹ Loo, kwenye nguvu hizo za Mungu nitakazofurahia nitakapopitia kwenye hizo barabara za dhahabu! Na huko,

maskini ile bunduki ya kale ambayo sasa inaning'inia ukutani, sitakuwa na haja nayo tena. Sijui, kama gari langu likija, kama maskini farasi wangu wa kusafiria niliyemwona katika ono atakuwa amefungiwa kwenye gari langu, asubuhi hiyo, amesimama kule mtoni. Ninatumaini yuko mtoni. Ninataka kutwaliwa juu. Ninataka kanisa litwaliwe juu namna hiyo pia, ninataka kila mmoja wenu.

¹²² Ungetaka kujua ni wakati gani utashuka kwenda Yordani? Utaacha mifumo hii isiyomcha Mungu ya ulimwengu huu na kumpokea Yesu Kristo kama Mwokozi wako? Endapo wewe si Mkristo, mwaweza kuinua mikono yenu na kusema, “Niombee, Ndugu Branham. Nitakapofika Yordani, . . .”? Mungu akubariki. Mungu akubariki. “Nitakaposhuka Yordani, ninataka kuchukua nguvu za Roho Mtakatifu juu yangu na kuyapiga hayo maji baridi, na kuvuka.”

¹²³ Unawezaje kuketi chini ya matamshi kama hayo, upako wa Roho Mtakatifu, na ukijua ya kwamba Roho Mtakatifu huniambia hali yako, na ushindwe kuinua mkono wako? Inaonesha wakati umewadia wa ile safari ya nyikani! Je! kungekuwako na mmoja kabla hatujaomba, mwingine? Ni wawili tu walioinua mikono yao; watatu, Mungu akubariki, mwanangu.

¹²⁴ Baba yetu wa Mbinguni! Watatu; hilo litakuwa ni jambo zuri sana, Bwana, kama wao—watakuwa tu kule kwenye siku hiyo. Naomba ya kwamba watakuwako, Bwana. Waliinua mikono yao kwa maana wameshawishika ya kwamba mifumo hii ya ulimwengu inakufa, na sauti za Neno la Mungu hivi karibuni zitakuwa ni kitu kigumu kukipata, Mungu ataiondoa kanisani. Mlio, ule mwito wa Bwana Arusi utaondoka hivi karibuni na madhehebu ya Yezebeli yatausonga uishe. Lakini wao wanataka kuwa . . . kuishi kwenye kijito hicho kilichofichwa kama vile Eliya alivyokuwa ahifadhiwe katika wakati wa njaa. Mungu wape Roho Mtakatifu sasa, ijaze mioyo yao kwa furaha na amani, na uweke nia zao juu ya Neno la Mungu wapate kuishi sasa na baadaye, milele. Wabariki, Baba. Hao ni Wako, kwa Yesu Kristo Bwana wetu.

Huku vichwa vyetu vimeinamishwa:

¹²⁵ Hao walioinua mikono yao na wanataka kumkubali Kristo, mnaweza tu kusimama kwa miguu yenu, kwa muda kidogo tu, ninapowaomba mmoja mmoja? Simameni tu kwa miguu yenu.

¹²⁶ Ee Mungu, je! nimeshindwa? Hata hao watatu walioinua mikono yao, bila ya kushawishika kusimama kwa miguu yao kukubali jambo lile lile ambalo wanalofanya! Bwana Yesu, ninayakabidhi yote mikononi mwako. Nimehubiri Neno Lako, na bila kupatana ko kote. Sasa ni—ninawaachia ukumbi, Baba. Fanya lo lote unaloona linafaa kwa kanisa na mtumishi Wako, yote yako mikononi Mwako.

¹²⁷ Baba, ninaomba ya kwamba utawaokoa waliopotea, wajaze wenye njaa kwa vitu vizuri, wape Uzima wa Milele hao walio na kiu, wainue watumishi Wako kuutangaza Ujumbe, wape wagonjwa uponyaji na wanaoteseka, jipatie utukufu, kwa kuwa najikabidhi mwenyewe pamoja na Neno Lako. Na mkononi mwangu, na moyoni mwangu, na niani mwangu, andika Sheria Zako, katika Yesu Kristo Bwana wetu. Amina.

Nitakapofika mtoni mwishoni mwa siku,
(sitaimba wimbo huo.)

Na inaonekana kana kwamba marafiki wangu
wote wameondoka;

Kutakuwa na Mtu fulani akingoja
atakayenionesha njia,

Haitanilazimu kuvuka Yordani peke yangu.

¹²⁸ Je! ulisambaza kadi za maombi, Bill? Ninasikia kuchoka. Uligawa zipi leo? B? Uligawa A pia, sivyo? Vema, waite. B kwanza, moja ya . . . Kadi ya maombi B, namba moja. Tutaombea magonjwa yenu. B, namba moja, ni nani aliye nayo? Kadi ya maombi B, namba moja, mtu fulani huko nyuma kabisa. Njoo hapa, bibi. B, namba mbili, inua mkono wako. Bibi huyo? Namba tatu. B, namba tatu, unaweza kuinua mkono wako tafadhali, kusudi niweze kuona ni wapi. Tatu? Namba nne, B, namba nne. B, namba tano. Unaweza kuinua mkono wako, tafadhali, B, namba tano. Mtu huyo? Vema, sita, saba, nane, tisa, kumi, kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu. Vema, hapa, hebu B zote na zisimame, hata hivyo, papo hapo zote zimekwisha. Kila mmishenari hudumani, po pote wawezapo.

¹²⁹ Kadi zote za maombi B wasimame na mchukue nafasi zenu kulingana na namba zenu. Sasa, zilizokuwa zinafuata zilikuwa ni zipi? A? Ni nani aliye na kadi ya maombi A, moja? A, moja, iko wapi? Hakika iko humu. A, moja? Zimetolewa siku mbili, ama tatu sasa, kwa hiyo huenda wasiwe hapa. Wote walio na kadi ya maombi A, sasa fanyeni mstari upande huu. Nendeni moja kwa moja kwenye ukuta, kwa uchaji.

¹³⁰ Ninataka kuzungumza nanyi msio na kadi za maombi, dakika moja kabla mstari haujaanza.

¹³¹ Sasa, ukiwa na kadi yako ya maombi, ishike mkononi mwako kusudi vijana waweze kuipokea, kadi yako ya maombi. Umekuwa ukingoja, umekuja mapema jioni kuchukua kadi yako ya maombi, nawe una haki ya kuingia mstarini. Niliahidi, kuwaombea. Sasa nitajaribu kutimiza ahadi yangu, Mungu akinisaidia.

¹³² Je! huyo ni mvulana wako mdogo? Mtu mdogo mwenye sura nzuri sana. Naomba unisamehe. Mwanamke huyu hapa ni mfano mzuri wa Mmarekani halisi. Mvulana wake mdogo, ovaroli ndogo na jaketi iliyo na milia. Kijana mwanamke mwenye nywele ndefu, anavalia vizuri. Mungu ambariki pamoja na

nyumba yake, na mumewe na wapendwa wake. Hiyo kweli ni Marekani halisi, yenye kuandikwa “Ukristo” hapo juu. Nchi yetu na idumu hivyo kwa muda mrefu! Samahani, maskini bibi, kwa kusema jambo hilo, lakini mimi ninaninii tu. . . ili kwamba watu waweze kuona kile ninachofikiria kinaonekana kama Mkristo; hakuna rangi za makucha, sijui kitu hicho ni nini, bibi tu.

¹³³ Mungu akubariki, Ndugu Sullivan.

¹³⁴ *Ni Tabibu*, tafadhali.

Ni tabibu wa Karibu,
Yesu mwenye huruma;

¹³⁵ Je! mnamwamini? Mnaamini ya kwamba Yeye ni Tabibu Mkuu wa Karibu? Sasa hebu iweni na uchaji kwa muda kidogo tu. Tungali tuna wakati mdogo, nilifupisha ujumbe kidogo tu. Natumaini mliupata, hata hivyo, kile kilichomaanishwa. Amini tu kwa moyo wako wote. Wote wamepangwa kwenye mstari, mtu fulani huko nyuma wa kuwapanga watu. Sawa? Sasa wote walio na kadi za maombi wamesimama.

¹³⁶ Je! mnaamini huko nje, pia, msio na kadi za maombi? Kama mtakuwa na imani, Mungu atawaita *ninyi*. Sasa, kadi zote za maombi wasimame mstarini.

¹³⁷ Huyo msichana mdogo anayeketi pale nyuma, anayeumwa mguu, hapa kwenye hii. . . Je! unaamini ya kwamba Mungu atauponya? Kama unaamini, uwe na imani tu na Mungu atakujalia hilo.

¹³⁸ Unafikiri baba yako mgonjwa atakuwa mzima? Utaamini, na liwe lako.

¹³⁹ Vipi wewe kule nje, unayemwombea mpwa wako aliye na ugonjwa wa wasiwasi? Unafikiri Mungu atamfanya mzima? Bibi, unayeketi kule, kama unaamini jambo hilo, unaweza kulipokea.

¹⁴⁰ Ninyi nyote mtaamini?

¹⁴¹ Sasa nataka. . . Ni wangapi walio ndugu zangu wako hapa, wahubiri wa Injili, wahubiri wa Full Gospel ama wo wote wale, wanaoamini katika kuponya Kiungu? Inueni mikono yenu. Ningewatakeni mje hapa na kunisaidia kuwaombea watu hawa, ili kwamba watu waweze kuona ya kwamba si mimi tu ninayewaombea watu, ninyi pia mnaweza kufanya hivyo. Njoni hapa na msimame jukwaani pamoja nami. Mnaweza kufanya hivyo, ndugu, ninyi wahudumu? Njoni papa hapa na msimame jukwaani. Naam. Asanteni, ndugu. Asanteni. Njoni moja kwa moja ndugu, njoni.

¹⁴² Ati nini? [Mtu fulani anasema, “Tunaweza kufanya mistari miwili hapa?”—Mh.] Naam, mnaweza. Fanyeni mistari miwili papa hapa, itakuwa vizuri. Hilo ni sawa. Sasa angalieni upande huu mwingine, ndugu. Geukeni hivi, nitawaleta watu moja kwa moja kupitia hapa. Sasa baadhi yenu njoni upande huu wangu, papa hapa, simameni upande huu. Namna hiyo.

¹⁴³ Sasa, kwa wasikilizaji, mnaona watu hawa wazuri hapa? Ni watu watakaosimama moja kwa moja hapa, na kuitetea Injili hii hii ninayohubiri. Mnaona? Wanakuja hapa kwa sababu wanaiamini. Sasa mnapaswa kujivunia mchungaji wenu atakayejitokeza kwenye jukwaa hili hapa, mahubiri magumu, makali. Hawa ndio watu walio na ufunuo, wanaojua ya kwamba...si kwamba mimi niko dhidi ya mtu huyo, mara nyingi tunafungwa kwenye madhehebu ambayo hutufanya sisi...Sisi tunachopinga ni hiyo mifumo; sio huyo mtu, mtumishi wa Mungu.

¹⁴⁴ Sasa, kama tungelikuwa na utambuzi kwa kila mtu hapa, unafikiri ningekuwa hapa kwa muda gani? Ngingezimia nikifikia kama...baada ya watu kama sita, watano ama sita, kumi; kidogo zaidi, labda nusu, robo ya mstari, ningekuwa nimekwisha, hao wengine hawangeombewa. Hatuwezi kufanya jambo hilo. Na kama ni...lakini si lazima uwe nao. Unajua shida yako ni nini. Unajua uliyofanya, sasa tubu dhambi zako. Kama ye yote wenu huko ana hata chembe moja ya mashaka moyoni mwako, iondoe sasa hivi na umwambie Mungu akusamehe. Kama wewe huko sawa na Mungu, mwambie Mungu akusamehe. Kama humwambii, nawe si sawa na Mungu, haitakusaidia hata kidogo kupitia hapa. Unapoteza wakati wako tu. Hiyo ni kweli. Sasa, hiyo ni kweli, ndugu? [Ndugu wanasema, "Amina"—Mh.] Hiyo ni kweli.

¹⁴⁵ Angalia hapa. Huyu hapa Ndugu Kidd amesimama hapa. Karibu nirarue tairi za gari langu nipate kufikia alipo, kama mwaka mmoja ama miwili iliyopita, kuninii... Alikuwa anakufa kwa kansa, yuaenda kufa siku hiyo. Mkewe aliniambia, akasema, "Hima!" Kasema, "Yeye anakufa sasa." Nilipofikia hapo, Bwana akamponya. Naye huyu hapa angali anasimama. Nafikiri uzito wake umeongezeka *sana* na kila kitu. Shujaa wa zamani, amerudi, wajua. Nilikuwa nikizungumza juu ya mtu wa aina hiyo, miaka kadha iliyopita, aliyehubiri; na akakaa moja kwa moja kwenye Neno hilo, na watu wakamcheka. Na yeye pamoja na mke wake wakitembea kwenye njia za reli na cho chote kile, na huko juu sana milimani, na kwenye mashimo ya makaa, na kufukuzwa, na kutupwa gerezani, na cho chote kile. Huyu ndiye mtu yule ambaye amepigana kupata thawabu, ni mtu wa aina hiyo.

¹⁴⁶ Sasa, ndugu, ninawaambia, huenda msiwe na roho ya utambuzi. Si lazima hiyo iwepo, unaona, hiyo—hiyo si muhimu. Jambo la kwanza, wewe ni mtu wa Neno. Ninyi ni bora zaidi, wahubiri bora kuliko nilivyo mimi, kwa maana mimi—mimi si muhubiri sana. Lakini ni...lakini ninyi m—mna upako, mtu ye yote aliyetwa kuihubiri Injili ameitwa kuwaponya wagonjwa; maagizo ya kawaida ni: "Enendeni ulimwenguni kote na mkaihubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokolewa. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.

Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, na kadhalika, watapata afya.” Kama umeitwa kuwa mhudumu, umeitwa kuwaombea wagonjwa.

¹⁴⁷ Na sababu ya mimi kufanya jambo hili ni kusudi wasikilizaji hawa... wapate kuona ya kwamba haiwabidi kumngojea mtu maalum, Oral Roberts, Tommy Hicks, Tommy Osborn, mimi mwenyewe, mtu fulani anayekuja kwa ajili ya ibada ya kuponya. Ninawataka waone ya kwamba ninyi ni watu wa Mungu. Mnaona? Wewe ni mtu... mna haki ya kuweka mikono yenu juu ya ye yote wao kama—kama mimi ama mtu mwingine. Hata hivyo, ndugu, nyote mnajua, kama—kama wahudumu, ni imani yao wenyewe katika Mungu inayotenda kazi. Hiyo ni kweli? Tunafanya maombi tu kwa ajili yao.

¹⁴⁸ Sasa unasema, “Ndugu Branham, je! Roho, ama Roho Mtakatifu yuko hapo pamoja nawe?” Kabisa. Naam, bwana!

¹⁴⁹ Sasa kwako wewe uliyeko huko kwa wasikili... huko kwenye mstari, kama unaamini kwa moyo wako wote ya kwamba Mungu atawaponya, inua mkono wako, useme, “Nitakubali.”

¹⁵⁰ Sasa, njoni hapa, hebu huyu—hebu bibi huyu hapa aje. Mimi sikufahamu, sijapata kukuona. Kama Roho Mtakatifu ataniambia, ili kwamba ndugu zangu hapa, walioko hapa namna hii, kwa hiyo wote wanasimama kunizunguka mimi hapa. Na si hivyo tu, ndugu zangu wako hapa, na Bwana wangu yuko hapa. Ni Bwana wao, pia. Sasa, kama ataniambia jambo fulani kasoro kwako, kasoro yo yote uliyo nayo, utajua kama ni kweli ama si kweli. Ninawataka, ninataka wasikilizaji, ninawataka watu huko nje waone ya kwamba Roho Mtakatifu yuko hapa jukwaani kutoa utambuzi, lakini jambo hilo halimponyi mtu ye yote. Lakini kama Yeye ataniambia jambo fulani kukuhusu wewe, ambalo wewe unajua sijui kitu cho chote juu yake, kama tu ilivyokuwa kwa yule mwanamke kisimani... Si kisa cha aina ile ile, bali ninamaanisha mwanamume na mwanamke wakikutana kwa mara ya kwanza. Yesu, akiwa kwa namna fulani mtu wa makamu, na mwanamke huyu labda alikuwa ni kijana mwanamke, labda kama wewe.

¹⁵¹ Na kama atafanya jambo hilo, angeweza kuniambia uko hapa kwa sababu gani, shida yako, je! ungeamini ya kwamba haina budi kuwa ni Roho Wake ambaye angefanya jambo hilo? Enyi ndugu mnaamini jambo hilo? Ya kwamba Yesu yeye yule anasimama hapa? Ninyi wasikilizaji mnaamini jambo lile lile? Ninyi mlio kwenye mstari wa maombi mnaweza kuamini jambo lile lile, na mjue ya kwamba watu hawa...? Je! ningeweza kuwaita hapa kama ningalifikiri hawakuwa...? Baada ya kuhubiri namna hii, na kusema mambo niliyosema, halafu niwaite watu hapa ambao hawakustahili? Nisingefanya jambo hilo. Ningekuwa nikipinga jambo lile lile nililokuwa nikinena habari zake. Unaona. Ninawaamini. Ninaamini hao ni watu wa Mungu.

¹⁵² Sasa angalia kama Roho Mtakatifu anasimama karibu. Kuzungumza nawe tu, ninajaribu... Unasema, “Unafanya nini, Ndugu Branham?” Jambo lile lile alilofanya Yesu kwa mwanamke yule, kasema, “Nipe maji ninywe,” Yeye alikuwa tu akijaribu kuzungumza naye kwa muda kidogo, apate kujua shida yake ilikuwa ni nini.

¹⁵³ Shida yako ni wasiwasi, huo ndio unaokusumbua. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Sasa, kwa kweli yeye haonekani yuko hivyo. Sivyo, ndugu? Haonekani, lakini hiyo ndiyo shida yake. Amekuwa hivyo muda mrefu. Daima unavuka daraja zako kabla hujazifikia, na kadhalika. Hiyo ni kweli. Ni maumbile yako, umeumbwa tu namna hiyo, wasiwasi; daima unawazia jambo fulani liko karibu kutokea, halikupati. Mara nyingi Ibilisi anakwambia, “Huna lo lote, wewe umerudi nyuma kabisa, umevuka mstari.” Mimi sisomi mawazo yako, lakini ninasoma jambo ambalo... Ninajua yale yeye alikuzungumzia, maana ninaona yale yaliyopitia mawazoni mwako.

¹⁵⁴ Sasa, Yesu alikamata mawazo yao. Hiyo ni kweli? Vema, hilo ndilo lililotukia sasa hivi. Hiyo ni kweli? Hapa, hebu nikwambie jambo fulani, kusudi upate kujua. Kwa kweli unasimama hapa kwa ajili ya mtu mwingine. Hiyo ni kweli. Haya basi, unaona, usingeweza kulipata mpaka wakati huo. Sasa, kama Bwana atanifunulia mimi ni kwa nini unasimama hapa, kwa ajili ya mtu mwingine, utaamini mimi kuwa ni nabii Wake? Ni kwa ajili ya mama yako. Unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yake ni nini? Vema, yeye ana shida ya moyo, msukumo mkubwa wa damu, vijiwe vya nyongo, matatizo. Hiyo ni kweli. Sivyo? Sasa? Huyu ni Roho Mtakatifu. Sivyo?

¹⁵⁵ Sasa, kuna kitu Fulani hapa kwangu na kwa ndugu hawa. Mnaona? Kitu fulani hapa sasa, Roho Mtakatifu. Sasa, aminini; ninyi, tunapopitia mstarini.

Hebu sote na tuinamisha vichwa vyetu tunapowaombea watu hawa:

¹⁵⁶ Baba yetu wa Mbinguni, tutawawekea mikono watu hawa. Nami ninawaombea sasa. Hawa hapa watumishi wako waaminifu wamesimama hapa, nasi sote tutaweka mikono yetu juu ya wagonjwa, kwa maana Wewe ulisema tufanye jambo hilo. Tutafanya hivyo katika Jina la Yesu Kristo. Jalia watu wasipite tu polepole, bali na wapitie hapa wakiponywa katika Jina la Yesu Kristo. Amina!

¹⁵⁷ Bwana akubariki. Sasa tembea uje papa hapa karibu. Katika Jina la Bwana Yesu, mponye... Katika Jina la Bwana Yesu, mponye ndugu yangu. Katika Jina la Bwana Yesu, mponye dada yangu.

¹⁵⁸ Sasa, hebu—hebu kidogo, unaona. Ndugu, dada, ni kwa nini mnafurahi wakati mwanamke huyo, wakati utambuzi ulipotukia, na wakati wengine wanapopitia hapa hakuna kitu

kinachotendwa? Watu wanapitia hapa, “Vema, kama mimi sininii. . . sitapata utambuzi, vema, basi sikupata kitu.” Hilo halina uhusiano wo wote na jambo hilo, Yeye yuko hapa vile vile. Unaona?

¹⁵⁹ Unapopitia hapa, njoo umeinua mikono yako, ukisema, “Asante, Bwana Yesu. Ninakukubali kama Mponya wangu, nami ninaondoka nikienda tu moja kwa moja nao. Mmoja wa watu hawa atanibatiza, nitaingia moja kwa moja katika kidimbwi cha maji na kubatizwa, na kutoka na kujua ya kwamba Wewe umeahidi ya kwamba nitampokea Roho Mtakatifu.”

¹⁶⁰ Unaona, ni. . . upambanuzi ungalipo hapa. Ungali upo hapa, sawa tu na. . . Hapa, ni yupi? Mtu huyu hapa? Hunijui. Sivyo, bwana? Sikujui. Naweza. . . kama Mungu ataniambia shida yako ni nini, je! utaamini kwamba mimi ni nabii Wake, mtumishi Wake? Utaamini kwa moyo wako wote? Vema, bwana. Asante, bwana. Huyu ni roho nzuri sana, jambo zuri sana. Hata hivyo, umesimama hapa kwa ajili ya mtu mwingine. Hiyo ni kweli. “Ni mjukuu wako, ana polio, alianguka hivi majuzi na kuvunja mguu wake,” hiyo ni BWANA ASEMA HIVI! Hiyo ni kweli? Hiyo ni kweli! Nenda zako na ukaamini sasa, naye atapata afya.

¹⁶¹ Sasa, njoni mkiamini, kila mtu tu, njoni tu. . . [Wahudumu wanawaombea wagonjwa katika mstari wa maombi—Mh.]

Kibarikiwe kifungo kinachoifunga
Mioyo yetu katika upendo wa Kikristo;
Ushirika wa ndugu wenye nia moja
Ni kama wa huko juu.

Mbele ya kiti cha enzi cha Baba yetu,
Tunaomba kwa bidii;
Hofu yetu, tumaini letu, nia zetu ni moja,
Faraja yetu na taabu zetu.

¹⁶² Mungu atawashikilia, enyi watoto wadogo wa Mungu mliolemaa, vipofu, mliopindika. Enyi wahudumu wa Injili, mnajua hatuna nguvu za kuponya. Lakini Bwana wetu aliye Mkuu, tunajua yupo amesimama hapa na anaweza kufanya ishara, na kumhukumu Ibilisi ambaye amekufunga. Tunamlaani Ibilisi. . . ? . . . Tunalaani upofu. . . ? . . .

¹⁶³ Katika Jina la Yesu Kristo Mwana wa Mungu, tunaomba ya kwamba Mungu atawapa imani kuamini ya kwamba maombi ya imani yamewaokoa wagonjwa, na Mungu atawainua, nao watapata afya tena. Tujalie, Mwenyezi Mungu, katika Jina la Yesu Kristo.

¹⁶⁴ Sasa ninyi ndugu ondokeni hapo, simameni jukwaani. Endeeleni tu kuomba. . . ? . . .

¹⁶⁵ Ninyi wengine wote endeeleni kuomba sasa, wakati sisi. . . wahudumu wanawaombea, pia, sasa. Tunaomba, tunawawekea mikono.

¹⁶⁶ Baba wa Mbinguni...Kwenu ninyi huko nje kwenye wasikizi ambao hamkuingia kwenye mstari wa maombi, wekeaneni mikono ninyi kwa ninyi sasa. Wekeaneni mikono.

¹⁶⁷ Baba yetu wa Mibnguni, tunakuletea Wewe wasikilizaji hawa tunapofunga ibada hii na kampeni hii chini ya beramu ya Yeus Kristo, Kuhani Mkuu wa Mungu aliyetiwa mafuta, Imanueli, akiwa amesimma, aliyefufuka katika wafu, aliye hai daima kufanya upatanisho; Uwepo Wake mkuu sasa ukiwa pamoja nasi, Nguvu Zake takatifu juu yetu za kutufanya tuone maono, kutoa unabii, kuweka mikono juu ya wagonjwa. Neno la Mungu lisiloshindwa haliwezi kamwe kumrudia Yeye bure. Ninalaani kila ibilisi wa maradhi, kila nguvu ya dhambi, kila kutokuamini, katika Jina la Yesu Kristo, jalia ziwaache watu na jalia wawe wazima.

¹⁶⁸ Wabariki hawa ndugu wahudumu, Bwana, wakiwa wamekusanyika pamoja katika moyo mmoja na nia moja, na washiriki wote wa kanisa. Ee Mwenyezi Mungu, kwa huu Middletown mashuhuri, Ohio, tuma ufufuo baada ya haya, Bwana, utakaosambaa kila upande, kukusanyika pamoja kwa mifupa, Bwana, na mishipa ya ngozi. Na jalia nguvu za Mungu zinue kanisa kubwa lenye nguvu lililoshikana hapa katika mji huu ambalo litaeneza, kanisa la mfano, kila mahali nchini, ili kwamba watu wapate kuja katika mji huu kuona nguvu za Mungu. Tujalie, Bwana. Waponye wagonjwa na wanaoteseka, waokoe waliopotea, na ukipatie utukufu Mwenyewe.

¹⁶⁹ Tujalie hayo, ya kwamba vitambaa hivi vyote na vifurushi hivi vilivyo hapa...Ninaomba, Bwana, ya kwamba Roho Mtakatifu aliye juu yetu, na aliye ndani ya jengo hili akitutia mafuta, jalia kila mmoja wao apate afya. Imelandikwa katika Biblia ya kwamba wakati Israeli walipokuwa kwenye wajibu wao, wakienda zao kwenye nchi ya ahadi, ya kwamba Bahari ya Shamu iliingilia kati. Na mmoja wa waandishi alisema, "Mungu aliangalia kupitia hiyo Nguzo ya Moto ndipo Bahari ya Shamu ikaogopa na kurudi nyuma, nao Israeli wakaenda kwenye nchi ya ahadi ambayo iliahidiwa."

¹⁷⁰ Na sasa, liko katika Biblia, imeandikwa, "Ningetaka juu ya mambo yote ya kwamba upate afya." Na wakati lesi hizi zitakapowafikia watu, ambako Shetani ameweka Bahari ya Shamu mbele zao, naomba Mungu aangalie chini kupitia kwenye Damu ya Mwanawe, Yesu Kristo, na kuua kila ugonjwa kwa wale ambao hawakuweza kufika hapa; na maradhi na yaondoke na yaliogope Neno la Mungu na ahadi ya Mungu na upako wa Mungu, na jalia watu wapite waingine kwenye hiyo ahadi nzuri ya afya njema pamoja na nguvu. Tujalie, Bwana. Na tunakabidhi yote Kwako, katika Jina la Mwanao mpendwa, Mwokozi wetu Yesu Kristo. Amina.

Wasikilizaji:

¹⁷¹ Kwake Yeye atujuaye sisi sote, kwa Yeye aliyetuina tupate kuwa urithi Wake ulimwenguni, katika kanisa Lake, jalia baraka nyingi za Mungu ziwe juu yenu nyote mpaka tutakapoonana tena. Ibada yetu inayofuata, nijuavyo mimi, itakuwa kwenye maskani, Jumapili asubuhi, Jumapili asubuhi ya Pasaka. Ndipo nitaenda kuninii... huko Illinois kutoka hapo. Awabariki, hudhurieni makanisa yenu, hudhurieni makanisa haya mazuri, iweni katika moyo mmoja. Dumuni katika Neno la Mungu! Mwishieni, kwa maana mambo ya kutisha yako mbele zenu, kumbukeni jambo hilo!

¹⁷² Hata tutakapoonana, hebu na tusimame na kuimba.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza,
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

¹⁷³ Sasa, kwa uchaji, peana mikono na mtu aliye nyuma yako, mbele yako, na kando yako.

Nampenda, . . . (kila mtu, sasa) . . . Nampenda
Kwani alinipenda kwanza,
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

¹⁷⁴ Sasa huku mikono yenu imeinuliwa kwa Mungu, kwa sauti kuu sasa, kila mtu aifanye isikike:

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza,
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

¹⁷⁵ Na tuinamishe vichwa sasa:

Hata twonane huko juu,
Hata twonane Kwake kwema;

Kumbukeni, wengi wetu hatutakutana tena mpaka wakati huo.

Hata twonane huko juu,
Mungu awe nanyi daima.

¹⁷⁶ Sasa uvumisheni. [Ndugu Branham anaanza kuvumisha wimbo huo—Mh.] Mchungaji wenu.



DINI YA YEZEBELI SWA61-0319
(Jezebel Religion)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili alasiri, 19 Machi, 1961, katika National Guard Armory kule Middletown, Ohio, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Hii tafsiri ya Kiswahili ilichapishwa mwaka wa 2003 na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2003 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org